Jumatano Januari 1, 2025 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com

ISSN 0856 • Na. 0581909

LIKE & FOLLOW US 0677 020701 nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ The nipashe Digital nipashedigital

epaper.ippmedia.com MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii www.ippmedia.com




UKURASA 10

**MUME** adaiwa kujiua kwa sumu kisa kuibiwa fedha za malipo mkopo wa kausha damu



UKURASA 18

**BMH** yaokoa bilioni 1.6/- upandikizaji figo watu 50

## YALIYOMO

UKURASA WA 8

### ASAKWA KWA TUHUMA ZA KUCHOMA NYUMBA NA KUWAUA MAMA NA WANAWE WATATU

JESHI la Polisi mkoani Tanga linamsaka Mwita Yoba kwa tuhuma za kuchoma nyumba na kusababisha vifo vya watu wanne; ...

UKURASA WA 7

### MADEREVA 64 WA MABASI WAFUTIWA LESENI

MADEREVA 64 wa mabasi makubwa na madogo yanayotoa huduma za usafirishaji katika mkoa wa Kilimanjaro, wamefutiwa leseni kutokana na makosa ya mwendokasi...

UKURASA WA 24

### RAMOVIC: MCHEZO NA TP MAZEMBE NI HATIMA YETU LIGI YA MABINGWA

MAUAJI KADA CCM

### Makada CHADEMA waachiwa huru baada ya kusota rumande miaka 4

UKURASA 18

KARIBU 2025...

# Samia: Tumevuna haya mwaka jana

UKURASA 2




Rais Samia Suluhu Hassan

## Uchunguzi kashfa zabuni ya bil. 10/- wizarani waiva TAKUKURU

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) imekamilisha uchunguzi wa sakata la maofisa wa Wizara ya Maliasili na Utalii kuingilia zabuni ya Sh. bilioni 9.8 na kusababisha hasara kwa serikali.

Aprili 26, 2024, Nipashe iliripoti kuhusu hatua ya maofisa wa wizara hiyo kuingilia zabuni ya Sh. bilioni 9.8 katika Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA) na kusababisha hasara ya Sh. milioni 702 kwa serikali.

Kashfa hii ni miongoni mwa hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) zilizomo katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2022/23.

Kwa kutambua hilo, Desemba 23, 2024, Nipashe iliwasilisha maswali TAKUKURU, ikihitaji kujua hatua zilizochukuliwa dhidi ya maofisa waliosababisha hasara hiyo na sababu za

Endelea Uk. 3

MICHEZO SIMBA YAPAA KUFUATA POINTI TATU TUNISIA UK. 24 KATUNI UK. 6



Magari yakikwepa mawe yaliyowekwa na baadhi ya vijana eneo la Magubike wilayani Kilosa wakidai kuwekwa matuta katika barabara kuu ya Morogoro-Dodoma baada ya mmoja wao kugongwa na gari na kupoteza maisha juzi. **Habari Uk 7.** **PICHA: IDDA MUSHI**

# Samia: Tumevuna haya mwaka jana

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan ametaja mafanikio ya serikali yake kwa mwaka 2024, akijivunia kuvutia wawekezaji ambao miradi yao itazalisha ajira kwa watu 211,000 nchini.

Akihutubia kupitia vyombo vya habari vya Televisheni na Radio kufunga mwaka jana usiku, Rais Samia pia alisema ziara zake katika nchi 16 zimekuwa na tija kubwa, mojawapo ikiwa ni kuwezesha mafunzo ya urubani kufanyika nchini.

Katika ziara yake ya nchi ya Jamhuri ya Korea, akasema ilifanikisha kupatikana fedha zenye masharti nafuu Dola za Kimarekani bilioni 2.5 kwa ajili ya kutekeleza miradi katika sekta za maendeleo ikiwamo ujenzi wa kituo cha kisasa cha mafunzo ya reli.

Fedha hizo pia zitatumika kujenga chuo cha mafunzo ya anga na urubani, ujenzi wa kituo cha kusambaza umeme Nyakanazi, na kituo cha uchenjuaji wa madini na maabara za kisasa za vito, mradi wa uendelezaji wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na kutoa ajira kwa vijana.

Alisema ziara hiyo pia ilifanikisha kusainiwa mkataba wa masharti nafuu wa Dola za Marekani milioni 163.6 kwa ajili ya kugharamia mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Binguni na Kituo cha Mafunzo ya Afya huko Zanzibar.

Ziara ya nchini China ilifungua milango ya soko la bidhaa mbalimbali ikiwamo mihogo mikavu, soya, mabondo ya samaki, mazao ya baharini, asali, mashudu ya alizeti na pilipili na kuwasihi wakulima kuchangamkia fursa hiyo.

Alisema pia alishiriki mkutano wa viongozi wa nchi zenye Uchumi Mkubwa Duniani (G20), ambao pamoja na mambo mengine uliazimia kuunga mkono jitihada za upatikanaji wa nishati safi na uwekezaji kwenye kilimo ili kuondosha njaa na umaskini duniani.

**UCHUMI KUIMARIKA**

Aidha, alisema uchumi wa nchi uliendelea kuimarika na kuwanufaisha wananchi. Kati ya Januari hadi Juni 2024 ulikua kwa asilimia 5.4 ikilinganishwa na asilimia 4.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2023.

Alisema deni la taifa liliendelea kuwa himilivu, mfumuko wa bei ukibaki ndani ya lengo la asilimia tatu, hali iliyochangiwa na sera madhubuti za kifedha na ongezeko la uwekezaji ndani na nje ya nchi.

Alisema kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania, kati ya Januari hadi Novemba 2024, serikali ilisajili miradi ya uwekezaji 865 yenye thamani ya Dola za Kimarekani bilioni 7.7 inayotarajia kuzalisha ajira 205,000.

Alisema pia Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (EPZA), ilitoa vibali vya kuwekezwa nchini viwanda vipya vikubwa 15 vyenye thamani ya Dola za Marekani milioni 235, vinavyotarajia kuzalisha ajira karibu 6,000 na kuuza nje bidhaa zenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 94 kwa mwaka.

Alisema Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), imefanikiwa kukusanya Sh. trilioni 21.276 kati ya mwezi Januari na Oktoba, 2024 sawa na asilimia 99.3 ya lengo, likiwa ni ongezeko la asilimia 17.5 ikilinganishwa na makusanyo katika kipindi kama hicho mwaka 2023.

Alisema kuimarika kwa uchumi kumeiwezesha nchi kuendelea kufanya mabadiliko chanya katika mifumo ya elimu msingi, sekondari na vyuo vya ufundi, kusogeza huduma bora za afya karibu zaidi na wananchi na kusambaza umeme vijijini

Aidha, serikali imetekeleza dhamira ya kumtua mama ndoo kichwani, kwa kusimamia miradi 1,300 ya maji nchi nzima na kufikisha kutimiza lengo la asilimia 95 mijini na asilimia 85 vijijini.

Alisema serikali pia ilifanikiwa kuhamasisha kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, kuboresha mifumo ya masoko ya mazao mbalimbali, na kupata bei nzuri ya mazao kwa wakulima.

"Kwa mfano, kwa mwaka 2024 ufuta uliuzwa Sh. 4,850 kwa kilo ikilinganishwa na Sh. 3,600 mwaka 2023, kahawa aina ya arabika iliuzwa Sh. 8,500 kwa kilo ikilinganishwa na Sh. 6,500 mwaka uliopita na kwa kahawa aina ya robusta iliuzwa kwa Sh. 5,000 kwa kilo badala ya Sh. 3,500 mwaka 2023," alisema.

Alisema pia mbaazi iliuzwa Sh. 2,236 kwa kilo badala ya Sh. 2,000 mwaka 2023, kakao iliuzwa Sh. 35,000 kwa kilo ikilinganishwa na Sh. 29,500 mwaka uliopita na korosho iliuzwa kwa Sh. 4,195 mwaka 2024 ikilinganishwa na Sh. 2,190 mwaka 2023.

Alisema uzalishaji wa korosho unatarajiwa kufikia tani 425,205 kwa msimu wa 2024/2025 unaoendelea ikilinganishwa na tani 310,787 zilizozalishwa msimu uliopita wa 2023/2024.

Alitaja baadhi ya miradi ya kimkakati ambayo imeshaanza kutoa huduma kuwa ni Bwawa la Mwalimu Nyerere ambalo linazalisha umeme Megawatt 3,169 ikilinganishwa na mahitaji ya Megawatt 1,888 huku Reli ya Kisasa (SGR), ikitoa huduma kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma.

Alisema Shirika la Reli lililokuwa linasafirisha wastani wa abiria laki tatu hadi nne kwa mwaka ndani ya miezi mitano ya huduma za SGR, limesafirisha zaidi ya abiria 1,200,000.

Upande wa anga kumekuwa na mafanikio makubwa kutokana na mwaka huu Shirika la Ndege kufikisha ndege 16, kuongeza safari za ndani ya nchi na kimataifa kufikia 25, na kusafirisha zaidi ya abiria 1,1000,000 na tani 10,000 za mizigo.

Alisema serikali pia iliendelea kuboresha mifumo kwenye viwanja vya ndege na ujenzi wa viwanja vya ndege vya Arusha, Kahama, Mpanda na Songwe na mwakani inatarajia kukamilisha viwanja vya ndege vya Iringa, Mtwara, Songea, Kigoma, Msalato, Musoma, Shinyanga na Sumbawanga.

"Hapa nataka nisisitize kuwa, miradi hii ni yetu sote, na imejengwa kwa kutumia rasilimali zetu. Hivyo, tunawajibika kuitunza ili itunufaishe sisi na vizazi vijavyo kesho. Vitendo vya kuhujumu miradi hii ni kulihujumu Taifa," alisema.

Alihamasisha uwekezaji kwa njia ya ubia baina ya serikali na sekta binafsi (PPP) ili kuongeza ufanisi katika uzalishaji na huduma na mpaka sasa kuna jumla ya miradi 74 ya ubia ambayo ipo katika hatua mbalimbali za maandalizi na utekelezaji.

**ATHARI ZA KIMAZINGIRA**

Rais alisema katika kukabiliana na athari za mazingira kutokana na matumizi ya kuni, serikali ilizindua Mkakati wa Kitaifa wa Nishati Safi ya Kupikia na kuwaelekeza wahusika wasimamie ipasavyo utekelezaji wake ili kufikia lengo la asilimia 80 ifikapo mwaka 2034.

**CHANGAMOTO ZA 2024**

Rais alitaja changamoto serikali ilizokabiliana nazo mwaka 2024 kuwa ni athari za mvua za El-nino na Kimbunga Hidaya, iliyosababisha mafuriko, maporomoko na upotevu wa maisha, uharibifu wa makazi, mashamba na baadhi ya miundombinu ikiwamo barabara na madaraja.

Kutokana na hali hiyo taifa lilisimama pamoja kutoa misaada ya kibinadamu kwa wathirika huku serikali ikijenga nyumba 109 za waathirika wa maporomoko ya Hanang', mkoani Manyara."

Kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), serikali ilitumia Sh. bilioni 136 kutengeneza miundombinu iliyoathiriwa na kutenga Sh. bilioni 868 kutekeleza miradi 70 ya kujenga miundombinu katika maeneo mbalimbali yaliyoathiriwa.

Alitaja changamoto nyingine kuwa ni uhaba wa fedha za kigeni, hususan Dola ya Marekani iliyoathiri biashara na uwekezaji, serikali ilikabiliana nayo kwa kuunda kikosi kazi cha wataalam kilichotafiti hali hiyo na kushauri hatua za kuchukuliwa.

"Nafarijika kwamba, kufuatia utekelezaji wa mkakati huo, upatikanaji wa fedha za kigeni umeimarika. Aidha, katika kuchukua hatua za kuuhami uchumi wetu, serikali imefanya uamuzi wa kuweka akiba ya taifa ya dhahabu katika Benki Kuu ya Tanzania, ili kuongeza uhimilivu wa uchumi wetu."

Alitaja changamoto nyingine kuwa ni ajali ambazo kwa asilimia 97 zilitokana na makosa ya kibinadamu hasa uzembe wa madereva. Takwimu za Jeshi la Polisi Tanzania zinaonesha kuwa kati ya Januari hadi Desemba mwaka huu, kulitokea jumla ya ajali 1,735, kati ya hizo 1,198 zilisababisha vifo vya watu 1,715 wengine 2,719 wakijeruhiwa.

Aliiagiza Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Jeshi la Polisi Tanzania kuongeza mikakati ya kuzuia ajali zinazosababishwa na makosa ya uzembe.

Alisema pia serikali itajenga viwanja na kumbi zenye viwango vya kimataifa ili kuvutia michezo na mikutano ya kimataifa nchini pamoja na ujenzi wa viwanja unaoendelea Arusha na Dodoma kwa ajili ya kujiandaa na mashindano ya CHAN Februari 2025 na AFCON 2027 ambayo Tanzania ni mwenyeji.

Nchi hiyo imeendelea kusimamia utekelezaji wa falsafa ya 4R, inayohimiza maridhiano, ustahamilivu, mageuzi na kujenga nchi pamoja na kuendeleza uhuru wa habari, wa

kujieleza, kutoa maoni kupitia vyombo mbalimbali na wa kukusanyika na kujumuika.

**UCHAGUZI MKUU**

Rais Samia alisema kuwa mwaka huu ni muhimu kwa maendeleo ya kisiasa na demokrasia kwa sababu utafanyika Uchaguzi Mkuu kuwachagua rais, wabunge na madiwani na kwa upande wa Zanzibar, atachaguliwa rais, wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na madiwani.

Alisema miongoni mwa maandalizi yaliyofanyika ni kurekebishwa kwa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, na Sheria ya Vyama vya Siasa.

"Ni imani yetu kwamba sheria hizo zitatuongoza vyema katika kusimamia kwa ufanisi chaguzi zijazo. Nitoe rai kwa wananchi na wadau wote wa uchaguzi kuhakikisha tunaidumisha sifa ya nchi yetu ya kuwa na demokrasia iliyojengeka juu ya msingi wa uhuru na haki," alisema.

***Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga simu / sms / WhatsApp : +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

HABARI KITAIFA

# Uchunguzi kashfa zabuni ya bil. 10/- wizarani waiva TAKUKURU

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) imekamilisha uchunguzi wa sakata la maofisa wa Wizara ya Maliasili na Utalii kuingilia zabuni ya Sh. bilioni 9.8 na kusababisha hasara kwa serikali.

Aprili 26, 2024, Nipashe iliripoti kuhusu hatua ya maofisa wa wizara hiyo kuingilia zabuni hiyo katika Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA) na kusababisha hasara ya Sh. milioni 702 kwa serikali.

Kashfa hii ni miongoni mwa hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) zilizomo katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2022/23.

Kwa kutambua hilo, Desemba 23, 2024, Nipashe iliwasilisha maswali TAKUKURU, ikihitaji kujua hatua zilizochukuliwa dhidi ya maofisa waliosababisha hasara hiyo na sababu za kutokukamatwa kwao hadi sasa.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini - TAKUKURU, Doreen Kapwani, katika majibu yake kwa Nipashe jana, alisema:

"Suala hili linaendelea na uchunguzi na lipo katika hatua za kukamilisha maoni ya kisheria kabla ya kuwasilishwa kwa DPP (Mkurugenzi wa Mashtaka).

"TAKUKURU haijaona haja ya kuwakamata wahusika kwa kuwa wamekuwa wanatoa ushirikiano katika uchunguzi kila wanapotakiwa."



Jengo la makao makuu ya NCAA linalojengwa Karatu

**KASHFA ILIVYO**

Katika Ripoti yake ya Hesabu za Mashirika ya Umma kwa Mwaka 2022/23, CAG Charles Kichere anasema kuwa amebaini NCAA ilitoa zabuni Na. EA/055/2020-2021/HQ/W/01 kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya makao makuu ya mamlaka hiyo.

Zabuni hiyo ilipata mshindi Machi 9, 2022 baada ya kupitia mchakato wa kisheria kutekeleza mradi wenye gharama ya Sh. bilioni 9.8.

Hata hivyo, CAG anasema amebaini kuwa Aprili 21, 2022, yaani siku 43 baada ya mshindi kutangazwa, zabuni hiyo ilisitishwa kutokana na maelekezo ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Inaripotiwa na CAG kuwa NCAA ilielekezwa na wizara kusitisha zabuni hiyo na kuanza upya mchakato wa kuitangaza.

Hivyo, zabuni ilitangazwa upya Mei 6, 2022 na mzabuni yuleyule aliyeshinda awali alitwaa tena zabuni hiyo, safari hii thamani yake ikipanda kwa Sh. milioni 686.6 ndani ya miezi miwili kutoka Sh. bilioni 9.8 hadi Sh. bilioni 10.48. Gharama za mchakato mpya wa zabuni ni Sh. milioni 16.08, hivyo kusababisha hasara ya jumla ya Sh. milioni 702.68 kwa serikali.

Kifungu cha 27 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, SURA 418, kinamtaka CAG wakati wa ukaguzi, akibaini jambo lenye viashiria vya rushwa, atoe taarifa TAKUKURU.

Mnamo Aprili 25, 2024, Joseph Mwaiswelo, Mkurugenzi wa Elimu kwa Umma TAKUKURU, alikiri kuwa wakati CAG anakagua hesabu za NCAA kwa mwaka 2022/23, aliwapa taarifa za kubaini viashiria vya rushwa katika mchakato wa zabuni hiyo.

Mwaiswelo alisema wanachunguza baadhi ya watendaji wa NCAA na taasisi zingine za serikali kutokana na CAG kubaini viashiria vya rushwa kiutendaji katika zabuni hiyo.

***Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga simu / sms / WhatsApp : +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***






Mratibu wa mradi wa uchakataji wa chupa za plasitiki, mhandisi Onsphory Kamukuru (kulia), Ofisa Mazingira wa Jiji, Ally Mfinanga (wa pili kulia) na wa tatu kutoka kushoto ni Diwani wa Kata ya Chamwino, Jumanne Ngede, wakikabidhi vifaa vya usafi kwa wawakilishi wa vikundi vya usafi Kata ya Chamwino Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Ruwa'ichi: Tutashirikiana na TRA kuhamasisha wananchi kulipa kodi

**Na Mwandishi Wetu**

ASKOFU Mkuu Jude Thaddeus Ruwa'ichi, amesema Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Dar es Salaam litaendelea kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuhamasisha watu kulipa kodi.

Amesema watafanya hivyo kwa sababu suala hilo ni nyeti kwa maendeleo ya nchi.

Ruwa'ichi alisema hayo jana wakati akizungumza na Kamishna Mkuu wa TRA, Yusuph Mwenda, alipotembelewa nyumbani kwake, jijini Dar es Salaam.

Mwenda alimtembelea Askofu Ruwa'ichi ikiwa ni mwendelezo wa kuwashukuru walipakodi.

Askofu Mkuu Ruwa'ichi alisema suala la kulipa na kukusanya kodi linalohusu maendeleo ya nchi na ni sehemu ya wajibu wa kiraia.

Pia alifurahishwa na mfumo wa ukusanyaji wa kodi unaofanywa sasa na ukaribu ulioko baina ya TRA na wananchi.

"Kwa niaba ya Watanzania wenzangu, niwapongeze kwa kazi kubwa mnayoifanya. Niwahakikishie kwamba kadri ya nafasi na uwezo wetu, tutajitahidi kuwahimiza watu wazingatie na waenzi wajibu wa kulipa kodi kwa ajili ya maendeleo yao wenyewe.

"Ninafurahi kwa msisitizo ulioweka kwamba, katika kukusanya kodi hambagui huyu wala yule, mnatafuta kuwatendea wote haki, ninaomba hilo lidumishwe na litiliwe mkazo," alisema.

Askofu Mkuu Ruwa'ichi alisema TRA inafanya vizuri inapolenga kila raia kulipa kodi inayoendana na uwezo wa mtu husika na fedha hizo kutumika kwa ajili ya watu wote kuleta maendeleo bila kujali itikadi zao.

Kamishna Mkuu Mwenda alisema lengo la kumtembelea Askofu Ruwa'ichi ni kumshukuru kwa mchango wake katika kuhamasisha ulipaji wa kodi.



Mwenda alisema Desemba ni mwezi wa kuwashukuru walipakodi na kuzitaja baadhi ya taasisi zilizoko chini ya Kanisa Katoliki ambazo zimekuwa na mchango katika kodi.

Alizitaja taasisi hizo kuwa ni sekta za elimu na afya ambapo wakati mwingine wamekuwa wakisamehewa kodi kulingana na sheria za Kodi.

Mwenda alisema kulipa kodi kwa maslahi ya nchi ni jambo la kiimani kwa sababu zinapokusanywa huelekezwa katika shughuli za maendeleo zikiwamo elimu, afya na miundombinu.

***Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga / WhatsApp : +255 677 020 701 Email:customerrelations@guardian.co.tz***


KKKT DAYOSISI YA DODOMA OFISI KUU YA DAYOSISI

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA WA MAGARI

Katibu Mkuu KKKT Dayosisi ya Dodoma anawakaribisha Wananchi wote kwenye mnada wa hadhara wa magari saba (07) na trekta moja (01) utakaofanyika tarehe 18 Januari, 2025 Chuo cha Hekima Ipagala Dodoma Mjini na tarehe 25 Januari, 2025 Shule ya Sekondari Aya Wilaya ya Chemba. Orodha ya magari hayo na sehemu yalipoegeshwa imeoneshwa katika jedwali lifuatalo: -

| NA | AINA | NAMBA YA USAJILI | MAHALI LILIPO | HALI YA GARI |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Rav 4 old Model Petrol Engine | T602 AEA | Dodoma Mjini | Linatembea |
| 2. | Toyota Land Cruiser Prado - Diesel Engine | T809 BCG | Dodoma Mjini | Linatembea |
| 3. | Toyota Land Cruiser Hardtop - Diesel Engine | T134 AGU | Dodoma Mjini | Linatembea |
| 4. | Toyota Land Cruiser Hardtop - Diesel Engine | T691 AHD | Dodoma Mjini | Linatembea |
| 5. | Toyota Corolla - Petrol Engine | T523 BGF | Dodoma Mjini | Linatembea |
| 6. | Toyota Land Cruiser Hardtop - Diesel Engine | T131 AFY | Dodoma Mjini | Linatembea |
| 7. | Either Truck – Diesel Engine | T997 AGT | Chemba Dodoma | Halitembei |
| 8. | Tractor – Diesel Engine | T351 ECE | Dodoma Mjini | Linafanyakazi |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atalipa amana "deposit" isiyopungua 25% ya thamani ya gari / trekta alilonunua papo hapo na atakamilisha malipo yote ndani ya siku kumi 14 kuanzia tarehe ya mnada. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hilo atakosa haki zote za ununuzi na amana iliyolipwa haitarudishwa.
2. Mnunuzi atatakiwa kuchukua gari / trekta ndani ya muda wa siku saba (07) baada ya kukamilisha malipo.
3. Mnada utaanza saa nne (4:00) asubuhi katika kila kituo; na ruhusa ya kuangalia mali itatolewa kwa siku mbili (02) kabla ya tarehe ya mnada kuanzia saa 4.00 asubuhi hadi saa 10.00 jioni.

**Imetolewa na: Katibu Mkuu**
**KKKT Dayosisi ya Dodoma.**


# Mavunde apiga 'stop' uchimbaji madini mtoni

**Na Mwandishi Wetu,** CHUNYA

WAZIRI wa Madini, Anthony Mavunde, amesimamisha uchimbaji madini ya dhahabu kwenye Mto Zila hadi wataalamu wa mazingira watakapothibitisha kama hakuna madhara.

Alitoa msimamo huo juzi wa kusitisha shughuli hizo zinazofanywa na kampuni ya G & I Tech. Mining Company Ltd kwa kipindi hiki cha mvua za masika.

Awali, Mavunde alitembelea eneo la leseni ya mwekezaji huyo lililoko kijiji cha Ifumbo lililovamiwa na wananchi na kusababisha mgogoro na uharibifu wa mali.

"Tumetembelea maeneo yote mawili na sote tumejionea hali halisi ya mazingira. Ni dhamira na maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan kuona shughuli zote za kiuchumi hususani za madini zinafanyika kwa utulivu bila kuleta migogoro na pasipo kuathiri mazingira ya eneo shughuli zinapofanyika," alisema,

Mavunde alisema amesikiliza hoja za wananchi juu ya uharibifu wa mazingira huo, hivyo serikali itaunda timu ya wataalamu kufanya tathmini ya kina ya mazingira juu ya athari zinazoweza kutokea wakati wa uchimbaji wa madini.

Mavunde alisisitiza kuwa kwa sasa shughuli zote za uchimbaji madini zisimame kwa kipindi hiki cha mvua za masika kama Tume ya Taifa ya Kudhibiti Uharibifu wa Mazingira kutoka NEMC ilivyoelekeza.

Wakati Mavunde akitangaza uamuzi huo, wizara hiyo kwa kushirikiana na watalaamu wa mazingira na wananchi ilikuwa inakwenda kuunda timu ya pamoja ya kufanya tathmini ili iwaeleze kitaalamu iwapo shughuli za uchimbaji madini zinaweza kuendelea kufanyika pasipo athari kwenye mazingira katika mto huo.

"Nitumie fursa hii kuwataka wananchi wote kuacha vitendo vya uvunjifu wa amani na kujichukulia sheria mkononi, tunalaani kitendo cha kuvamia na kuharibu mali za mwekezaji," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mbarak Batenga, alishukuru ujio wa Waziri Mavunde na kusisitiza utaleta suluhisho la kudumu la mgogoro baina ya mwekezaji na wakazi wa Kijiji cha Ifumbo.

Batenga alisema serikali ngazi ya wilaya itaendelea kusimamia sheria na kanuni ili kuhakikisha eneo hilo linakuwa salama muda wote.

Mbunge wa Chunya, Masache Kasaka, kwa niaba ya wananchi aliishukuru serikali kwa namna inavyoshughulikia changamoto zao.

Alisema ombi la wakazi hao ni kuona mazingira ya Mto Zila yanatunzwa kwa kuwa ni chanzo kikubwa cha maji kwa wilaya hiyo.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alimshukuru Mavunde kwa kutembelea Chunya na kuahidi kusimamia maelekezo yake ya kuona shughuli za uchimbaji katika mto huo zinasimama kwa kipindi hiki ambacho mvua zinanyesha.

TANGAZO


KILIMANJARO
DRINKING WATER
A PRODUCT OF
The Coca-Cola Company
Mshindi wa
SUPERBRANDS
AFRIKA MASHARIKI
2022-2024
VOTED
Superbrands
EAST AFRICA'S CHOICE
2022-2024
Asanteni wateja wetu
Hii ni yetu sote
kilimanjaro_drinking_water
kilimanjarodrinkingwater
kdw@bbl.co.tz
+255 762628166 | +255 659785276 | +255 272754422

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mwaka Mpya wa 2025 uwe wa amani, upendo kwa Watanzania

**WATANZANIA** leo wanaungana na watu wa mataifa mengine duniani kusherehekea Mwaka Mpya wa 2025. Kwa ujumla, furaha hiyo inatokana na ukweli kwamba kwa neema ya Mungu, wamevuka mwaka 2024 salama salmini kwa kuwa wako ambao walianza nao mwaka lakini wametangulia mbele za haki.

Katika kusherehekea Mwaka Mpya, baadhi ya watu husherehekea kwa kufanya ibada ikiwa sehemu ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa matendo makuu aliyowatendea kwa mwaka mzima ikiwamo kuwapa neema ya kuvuka mwaka uliopita na kuingia mwaka mwingine.

Baadhi ya watu, katika kuaga na kuukaribiha Mwaka Mpya, wanafanya tathmini ya malengo waliyoyaweka mwaka uliopita ili kuona wamefanikiwa kwa kiasi gani na kwa baadhi ya mambo kuona ni vikwazo gani vilivyosababisha wasifikie matarajio yao na hatimaye kupanga mipango mipya kwa mwaka unaofuata.

Wakati hayo yakifanyika, watu katika medani za kijamii, kisiasa na kiuchumi, huangalia kwa kina, urefu na mapana mambo yaliyojitokeza mwaka uliopita na kujaribu kutoa ushauri nini kifanyike. Kama ni wanasiasa, wanajaribu kutathmini matukio makubwa yaliyotokea katika medani hiyo.

Mwaka 2024 kwa mfano, katika siasa, imeshuhudiwa kuwapo kwa mambo mbalimbali ukiwamo uchaguzi wa Serikali za Mitaa ambao ulifanyika Novemba na kuwapo kwa malalamiko mengi kwamba haukuwa huru na wa haki. Malalamiko hayo yalitolewa zaidi na wapinzani na wanaharakati waliosema mambo yaliyojitokeza katika uchaguzi wa mwaka 2019 yalijirudia tena na kusababisha hali hiyo.

Jambo lingine lililojitokeza na kupigiwa kelele na baadhi ya wanasiasa, viongozi wa dini na wanaharakati wa haki za binadamu ni matukio ya utekaji na mauaji na watu wengine kukamatwa na kupotea kusikojulikana. Lawama kubwa katika hilo pia zilielekezwa kwa serikali na vyombo vya ulinzi na usalama.

Huku hayo serikali ikitupiwa mzigo wa lawama, jinamizi la ajali za barabarani zilitikisa nchi nzima na kusababisha mamia ya watu kupoteza maisha na wengine wapata ulemavu wa kudumu wa viungo. Sababu kubwa kuhusu ajali hizo ni uzembe wa madereva kwa kushindwa kufuata sheria za usalama barabarani.

Kama wahenga wasemavyo hakuna jambo lisilokuwa na sababu, ni vyema kasoro hizo zilizojitokeza kwa mwaka 2024 kama vile uchaguzi kutokuwa huru na haki, watu kutekwa, kukamatwa na kuuawa na ajali za barabarani, ni vyema kila mtu, taasisi na serikali zilizopewa kazi ya kusimamia majukumu husika, zikasimamia haki na hatimaye iondokane na lawama katika masuala husika.

Mwaka 2025 kunatarajiwa kufanyika uchaguzi mkuu wa Rais, wabunge na madiwani kwa Tanzania pamoja na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar. Ni vyema Tume Huru ya Uchaguzi (INEC) na Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) zikahakikisha mchakato huo unafanyika kwa misingi ya uwazi bila upendeleo ili uwe huru na wa haki. Kwa maneno mengine, tume hizo zitangaze matokeo halisi ya uchaguzi badala ya chama fulani.

Kwa masuala ya watu kutekwa na wengine kuuawa, ni vyema serikali ikaimarisha ulinzi na usalama na pale panapotokea mauaji, uchunguzi ufanyike na wanaobainika au kutuhumiwa kuhusika wafikishwe katika vyombo vya sheria.

Kuhusu ajali za barabarani, kama ambavyo Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa akisisitiza kukomeshwa kwa matukio hayo, Jeshi la Polisi kupitia Kikosi cha Usalama Barabarani, likachukua hatua madhubuti kukomesha matukio hayo. Kama ni ubovu wa magari, ni vyema yakazuiwa kufanya safari ili kuokoa maisha ya watu.

Iwapo kila mmoja atasimama kikamilifu katika nafasi yake, ni dhahiri kwamba amani, upendo, umoja na mshikamano vinavyoimbwa kila siku vitashamiri na Tanzania kuendelea kuwa kisiwa cha amani. Mwaka mpya wa 2025 uwe wa amani na upendo kwa Watanzania.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Gaudensia Mngumi

# Tunakutakia 2025 yenye mafanikio

**LEO** Watanzania kote walipo majijini, mijini na vijijini wanakusanyika pamoja na familia na marafiki kuushangilia mwaka mpya.

Nipashe Mwanga wa Jamii inawataka wasomaji na watangazaji wetu na kila mtu heri ya mwaka mpya 2025.

Heri zetu zinaambatana na kuwatakia afya tele, furaha na mbinu mpya za utafutaji ili kuwa na maisha bora zaidi.

Huu daima ni wakati wa matumaini, tunapoadhimisha mwisho wa mwaka mmoja na mwanzo wa mwingine tuna matumaini kuwa mambo yatakuwa mazuri au sawa.

Na ingawa mwaka wa 2024 kwa wengine ulikuwa mgumu kwa gharama za maisha kuzidi kuongezeka, upatikanaji wa pesa pia kuwa mgumu na ughali wa chakula nao ni changamoto. Hilo halituyumbishi, tuna matumaini.

Hata hivyo, lazima pia tuangalie nyuma, tukiamini kuwa mwaka huu unaleta siku angavu zaidi tena ziko mbele yetu na kwamba ingawa changamoto zetu ni kubwa, kila mmoja wetu ana ujasiri na dhamira ya kuisimama na kukabiliana nazo 2025.

Ni roho hiyo ambayo imezifanya familia zetu na taifa kuwa hai na ni roho hiyo ambayo itaiweka hai nchi hii na sisi raia wake kwa vizazi vijavyo.

Wakati huu, tunatafakari juu ya nguvu inayotuweka pamoja kama raia na taifa letu la Tanzania.

Tunaitazama michango ya serikali kwa maendeleo yetu na sisi pia tuangalie michango yetu kwa maendeleo ya familia zetu na nchi pia.

Tujue kuwa huu ni wakati wa kujikumbusha kwamba kila mtu ni mchezaji kwa mafanikio ya nchi yetu. Si jukumu la serikali pekee na sisi pia.

Sisi ni taifa tajiri lenye rasilimali nyingi tuazimie tufanye kazi kwa uaminifu na uaminifu kwenye ngazi zote nyumbani, viwandani, ofisini, shambani na hata kwenye viwanja vya mpira na majukwaa ya burudani tubadilishe maisha yetu.

Ni lazima pia tujue kuwa tuna tamaduni na mila tofauti tunahitaji kuvumiliana na kushirikiana kujenga nchi yetu ili taifa liwe bora kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Ni lazima kutii sheria kuanzia za barabarani, za ardhi za elimu, kilimo na pia kupenda kutafuta taarifa sahihi ili tupate ufahamu na maendeleo.

Kupitia bidii, umoja, juhudi na uvumilivu na umoja Watanzania tushirikiane kuendeleza rasilimali na ujasiriamali, umiliki wa biashara na kuwa na fikra za kubadilika kuendeleza taifa bila kutegemea misaada na uhisani.

Kila mmoja ajengwe na imani kwamba Tanzania ni yetu na katika nchi hii kubwa yenye karibu watu milioni 65 na utajiri mwingi, yeyote anaweza kuifanya ikiwa bora zaidi hivyo ajaribu.

Aidha, kila mmoja awe kuwa mwaminifu kujenga taifa, kutunza fedha za umma, kusimamia na kujenga miradi bora kama shule, hospitali, miundombinu na mingine mingi ili kuwa na Tanzania bora zaidi.

Ndiyo maana ni muhimu zaidi kuliko mwaka jana kwamba tutajirekebisha ili kuwa na mawazo chanya na kupaza sauti zetu na kutumia fursa zilizopo kufikia maendeleo kwa wote.

Iwe unasherehekea mwaka wa 2025 ukiwa kazini, au bila kuwa na ajira, makazi bora au hata kama unaumwa kuwa na matumaini kwamba sote tunaweza kutafuta na kupata fursa na mafanikio.

Tunaweza kuibadilisha Tanzania sisi wenyewe siyo lazima awepo wa kutusaidia. Kwa hiyo mabadiliko yaanze na wewe.

Fikiria kuwa katika kufikia maendeleo mpe Mungu asilimia 75 na wewe ujibakizie asilimia 25.

Katika kufanya hivyo hutahangaika na ushirikina na kuwaua watoto, wanawake na wenye ulemavu. Utaacha uhalifu, utakuwa na hofu ya Mungu, hutaiba mali wala fedha za umma wala za watu kupitia mikataba au udanganyifu wowote.

Kadhalika kunyanyasa wengine kingono, utaacha uongo wala hutatamani mali za dhuluma na lolote linalokuingiza kwenye hatia.

Nipashe inakutakia wewe na wapendwa wako furaha, ustawi, afya njema na bahati katika mwaka mpya wa 2025.

**Heri ya Mwaka Mpya, kila mtu.**

HABARI KITAIFA

# Madereva 64 wa mabasi wafutiwa leseni

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MADEREVA 64 wa mabasi makubwa na madogo yanayotoa huduma za usafirishaji katika mkoa wa Kilimanjaro, wamefutiwa leseni kutokana na makosa ya mwendokasi, kusababisha ajali, ulevi na kuyapita magari mengine bila tahadhari.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Simon Maigwa, madereva wengi waliopoteza ajira zao ni waliosababisha ajali, kundi hilo likiwa na madereva 32 waliofutiwa leseni.

Alisema eneo lingine lililotikisa kwa makosa na kufutiwa leseni kati ya Januari hadi mwezi Desemba 2024, ni la madereva 22 waliokuwa wakitembea kwa mwendokasi.

Alisema madereva waliofutiwa leseni kwa sababu ya makosa ya kuendesha vyombo vya moto wakiwa wamelewa, ni watatu na waliokuwa wakivunja sheria za usalama barabarani kwa kuendesha na kuyapita magari mengine bila tahadhari (wrong overtaking), waliofutiwa leseni ni madereva saba.



Kuhusu matukio ya ukatili wa kijinsia kwa kipindi cha Januari hadi Desemba 2024, Kamanda Maigwa alisema makosa ya kubaka 42 yaliripotiwa.

Alisema kuwa makosa ya ulawiti yaliyoripotiwa ni 18. Makosa mengine yaliyoripotiwa ni manne ya kuwapa mimba wanafunzi sawa na idadi ya makosa ya ukatili dhidi ya watoto, hivyo kufanya jumla ya makosa kuwa 68.

Kati ya makosa hayo ya ukatili wa kijinsia, washtakiwa katika kesi hizo wamepewa adhabu ya kifungo cha maisha na wengine miaka 30 gerezani.

VURUGU ZA WANANCHI KILOSA:

# 27 wakamatwa kwa kufunga barabara kisa kifo cha kijana

**Na Mwandishi Wetu,** KILOSA

WATU 27 wanashikiliwa na vyombo vya ulinzi na usalama wilayani Kilosa, mkoani Morogoro kwa tuhuma za kufanya vurugu na kufunga barabara eneo la Magubike wilayani humo.

Inadaiwa wananchi hao walifunga barabara kuu ya Morogoro-Dodoma katika eneo hilo juzi, wakishinikiza serikali kuweka matuta kwenye eneo hilo baada ya kijana aliyefahamika kwa jina la Piason Senyagwa (20) kugongwa na gari na kupoteza maisha papohapo.

Akizungumza wakati wa mazishi ya kijana huyo aliyegongwa na gari na kupoteza maisha, Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, Shaka Hamdu Shaka alisema kuwa kutokana na vurugu hizo, mali mbalimbali zimeharibiwa na askari wawili kujeruhiwa.

Shaka aliwataka wananchi kuacha tabia ya kujichukulia sheria mkononi. Alisema kuwa tayari serikali inafanyia kazi changamoto hiyo.

Mkuu wa Wilaya huyo alisema kuwa miongoni mwa waliokamatwa, yumo dereva aliyehusika na ajali pamoja na gari lililosababisha ajali. Wanaendelea na taratibu zaidi za kisheria ikiwamo kufikishwa mahakamani.

Awali, Diwani wa Magubike, Abuu Msofe alisema kuwa siku ya tukio kijana huyo alikuwa anavuka barabara na kugongwa na gari.

Diwani huyo alisema kuwa kutokana na matukio hayo kujirudia mara kwa mara katika eneo hilo, wananchi wakajichukulia sheria mkononi kwa kufunga barabara kushinikiza serikali itatue changamoto hiyo kwa kuweka matuta.

Alisema kuwa baada ya kufunga barabara, askari polisi walifika katika eneo hilo na wananchi kuwarushia mawe na kufanya polisi kutumia mabomu ya machozi kuwatawanya wananchi.

"Kwa kipindi cha miaka miwili, watu tisa wamegongwa na magari katika eneo hili. Tunaomba serikali isikie kilio hiki na namna nzuri zaidi ya kusadia changamoto hii ambayo imedumu kwa kipindi kirefu," alisema diwani huyo.




airtel money

TUMA NA KUTOA PESA BILA TOZO

ADA ZA MIAMALA YA AIRTEL MONEY

TOA PESA KWA WAKALA/ATM

| Kutoka (TSH) | Kwenda (TSH) | Ada ya Airtel Money | Tozo ya Serikali | Jumla makato | Unalipa bila Tozo |
|---|---|---|---|---|---|
| 100 | 999 | 190 | 10 | 200 | 200 |
| 1,000 | 1,999 | 310 | 10 | 320 | 320 |
| 2,000 | 2,999 | 390 | 10 | 400 | 400 |
| 3,000 | 3,999 | 590 | 14 | 604 | 604 |
| 4,000 | 4,999 | 640 | 27 | 667 | 667 |
| 5,000 | 6,999 | 950 | 54 | 1,004 | 1,004 |
| 7,000 | 9,999 | 1,000 | 56 | 1,056 | 1,056 |
| 10,000 | 14,999 | 1,450 | 102 | 1,552 | 1,552 |
| 15,000 | 19,999 | 1,450 | 195 | 1,645 | 1,645 |
| 20,000 | 29,999 | 1,850 | 306 | 2,156 | 2,156 |
| 30,000 | 39,999 | 1,850 | 351 | 2,201 | 2,201 |
| 40,000 | 49,999 | 2,300 | 419 | 2,719 | 2,719 |
| 50,000 | 99,999 | 2,600 | 573 | 3,173 | 3,173 |
| 100,000 | 199,999 | 3,500 | 707 | 4,207 | 4,207 |
| 200,000 | 299,999 | 5,100 | 821 | 5,921 | 5,921 |
| 300,000 | 399,999 | 6,200 | 838 | 7,038 | 7,038 |
| 400,000 | 499,999 | 6,700 | 982 | 7,682 | 7,682 |
| 500,000 | 599,999 | 7,200 | 1,245 | 8,445 | 8,445 |
| 600,000 | 699,999 | 7,600 | 1,532 | 9,132 | 9,132 |
| 700,000 | 799,999 | 7,600 | 1,700 | 9,300 | 9,300 |
| 800,000 | 899,999 | 7,600 | 1,750 | 9,350 | 9,350 |
| 900,000 | 1,000,000 | 7,600 | 1,776 | 9,376 | 9,376 |
| 1,000,001 | 3,000,000 | 7,600 | 1,875 | 9,475 | 9,475 |
| 3,000,001 | 5,000,000 | 9,500 | 2,000 | 11,500 | 11,500 |

TUMA PESA AIRTEL - AIRTEL (BILA TOZO)

| Ada ya Airtel Money | Tozo ya Serikali | Jumla makato |
|---|---|---|
| 10 | - | 10 |
| 25 | - | 25 |
| 25 | - | 25 |
| 40 | - | 40 |
| 50 | - | 50 |
| 120 | - | 120 |
| 140 | - | 140 |
| 325 | - | 325 |
| 350 | - | 350 |
| 360 | - | 360 |
| 375 | - | 375 |
| 380 | - | 380 |
| 675 | - | 675 |
| 940 | - | 940 |
| 1,200 | - | 1,200 |
| 1,450 | - | 1,450 |
| 1,450 | - | 1,450 |
| 2,100 | - | 2,100 |
| 3,100 | - | 3,100 |
| 3,100 | - | 3,100 |
| 3,250 | - | 3,250 |
| 3,300 | - | 3,300 |
| 4,000 | - | 4,000 |
| 4,000 | - | 4,000 |

TUMA PESA MITANDAO MINGINE (BILA TOZO)

| Ada ya Airtel Money | Tozo ya Serikali | Jumla Makato |
|---|---|---|
| 10 | - | 10 |
| 45 | - | 45 |
| 45 | - | 45 |
| 90 | - | 90 |
| 90 | - | 90 |
| 180 | - | 180 |
| 180 | - | 180 |
| 495 | - | 495 |
| 495 | - | 495 |
| 540 | - | 540 |
| 612 | - | 612 |
| 675 | - | 675 |
| 1,125 | - | 1,125 |
| 1,440 | - | 1,440 |
| 1,710 | - | 1,710 |
| 2,070 | - | 2,070 |
| 2,250 | - | 2,250 |
| 2,880 | - | 2,880 |
| 3,870 | - | 3,870 |
| 3,870 | - | 3,870 |
| 3,870 | - | 3,870 |
| 5,400 | - | 5,400 |
| 5,400 | - | 5,400 |
| 5,400 | - | 5,400 |

LIPA KWA AIRTEL MONEY (BILA TOZO)

| Ada ya Airtel Money | Tozo ya Serikali | Jumla Makato |
|---|---|---|
| 20 | - | 20 |
| 50 | - | 50 |
| 70 | - | 70 |
| 100 | - | 100 |
| 200 | - | 200 |
| 300 | - | 300 |
| 500 | - | 500 |
| 500 | - | 500 |
| 850 | - | 850 |
| 920 | - | 920 |
| 1,000 | - | 1,000 |
| 1,200 | - | 1,200 |
| 1,700 | - | 1,700 |
| 2,000 | - | 2,000 |
| 2,600 | - | 2,600 |
| 3,000 | - | 3,000 |
| 3,300 | - | 3,300 |
| 4,500 | - | 4,500 |
| 5,500 | - | 5,500 |
| 5,700 | - | 5,700 |
| 6,000 | - | 6,000 |
| 6,000 | - | 6,000 |
| 6,000 | - | 6,000 |
| 6,000 | - | 6,000 |

TUMA PESA KWENDA BANK (BILA TOZO)

| Ada ya Airtel Money | Tozo ya Serikali | Jumla Makato |
|---|---|---|
| 140 | - | 140 |
| 220 | - | 220 |
| 400 | - | 400 |
| 450 | - | 450 |
| 600 | - | 600 |
| 710 | - | 710 |
| 1,000 | - | 1,000 |
| 1,250 | - | 1,250 |
| 1,430 | - | 1,430 |
| 1,430 | - | 1,430 |
| 1,930 | - | 1,930 |
| 2,120 | - | 2,120 |
| 2,780 | - | 2,780 |
| 3,740 | - | 3,740 |
| 4,600 | - | 4,600 |
| 4,700 | - | 4,700 |
| 5,200 | - | 5,200 |
| 5,400 | - | 5,400 |
| 5,400 | - | 5,400 |
| 5,500 | - | 5,500 |
| 5,500 | - | 5,500 |
| 5,500 | - | 5,500 |
| 7,500 | - | 7,500 |
| 9,000 | - | 9,000 |

FANYA MALIPO KWA AIRTEL MONEY

GePG MALIPO YA SERIKALI · LUKU · VING'AMUZI · MAJI · POLISI · SOLAR · BIDHAA MITANDAONI · MIAMALA YA KIBENKI · TRA · BRELLA · ARDHI · NDEGE · BIMA · VIKOBA · LIPA MITANDAO YOTE

Fanya yote na My Airtel App!
Pakua katika simu yako.

Download on the App Store · ANDROID APP ON Google play

Fanya malipo ya Serikali na bili mbalimbali kupitia My Airtel App

SUMATRA · Wizara ya Nishati na Madini · BRELA · Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi · dawasco

KUMBUKA

- Unaweza kuweka ama kupokea hadi Tsh 10,000,000 kwa siku na unaweza kutoa ama kutuma hadi Tsh 5,000,000 kwa siku kama usajili wako umekamilika na Airtel Money.
- Kila mara unapotuma pesa, kumbuka kuhakiki namba ya mpokeaji kuepuka kukosea na usumbufu.
- Airtel Money huonesha salio kwenye kila muamala. Endapo utafanya muamala wa kuangalia salio, kuangalia miamala miwili ya mwisho, taarifa ya muamala, muhtasari wa siku iliyopita, muhtasari wa siku, miamala ya mwezi uliopita, utatozwa gharama ya Tsh 50 kwa kila muamala.
- Kuwasiliana na Huduma kwa Wateja, Piga 100 bure au tembelea duka lolote la Airtel Money Branch.

Decemba, 2024

HARAKA.SALAMA.BILA MIPAKA.



Muuguzi wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete, Fatma Suedy, akimhudumia mmoja wa mwenye ulemavu wakati wa hafla ya kutoa misaada kwa makundi maalum iliyoandaliwa na Taasisi ya Mama Ongea na Mwanao Dar es Salaam jana katika viwanja vya Karimjee. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Serikali yawapa bilioni 6.8/- wananchi wahame hifadhini

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI imetoa Sh. bilioni 6.8 kwa ajili ya fidia kwa wananchi wanaoishi katika kijiji cha Ngombo, wilayani Malinyi, mkoani Morogoro kilichomo ndani ya Pori la Akiba Kilombero ili wahamie maeneo mengine nje ya hifadhi hiyo.

Ofisa Maliasili Mkoa wa Morogoro, Joseph Chuwa alisema hayo wilayani Malinyi jana wakati wa ufuatiliaji taratibu za wananchi kuhama maeneo yao na jinsi walivyoingiziwa fedha zao kwenye akaunti za simu zao ikiwa na kutatua changamoto ndogo kwao.

Chuwa alisema kuhamisha watu katika hifadhi hiyo kulianza miaka miatatu iliyopita kwa kuhamasha watu kupisha uhifadhi kupitia vikao mbalimbali hadi ngazi za chini.

“Katika kipindi hiki tupo kwenye kutekeleza zoezi hili na linaendelea vizuri. Watu wana amani na wamejiandaa siku nyingi kwenda kuhamia sehemu ambayo wameichagua,” alisema Chuwa.

Alisema wananchi wa kijiji cha Ngombo wanashukuru serikali kwa kuidhinisha fedha za fidia, kila mlengwa ameingiziwa katika akaunti yake kiwango anachostahiki.

“Wananchi wengi wao hawakuamini kama wangelipwa fidia na tena kwa haraka na tayari wameanza kubomoa nyumba zao na kuhama kwa hiari ili kuondoka kupisha uhifadhi kwenye eneo hili muhimu kwa shughuli za uhifadhi,” alisema Chuwa.

Alisema eneo la kijiji cha Ngombo lenye ardhi oevu linategemewa kuongeza wingi wa maji katika Mto Rufiji ili kusaidia maji kuzalisha umeme katika Bwawa la Nyerere pamoja na kurudisha wanyama mbalimbali wakiwamo adimu.

“Katika eneo la hifadhi, wamo wanyama adimu ambao ni pamoja na sheshe ambao kwa asilimia 70 duniani wanapatikana Bonde hili la Kilombero,” alisema Chuwa.

Alisema kijiji cha Ngombo kinapakana na mito mkubwa miwili ambayo ni Mpanga na Mnyera ambayo katikati yake ni kama kisiwa.

Chuwa alisema uamuzi wa serikali umewasaidia wananchi hao kuepuka nyakati za mafurukio ambayo yaliathiri robo ya kijiji na wakazi wake walilazimika kutumia mitumbwi, shule zilikuwa zinafungwa na kusababisha kuwapo mazingira hatarishi.

Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), Jonas Makwati alisema kuwa eneo la Ngombo limo ndani ya Hifadhi ya Kilombero.

Makwati ambaye ni Kamanda Mhifadhi Nyanda za Juu Kusini wa mamlaka hiyo, alisema Hifadhi ya Kilombero ni pori jipya lililoanzishwa na serikali mwaka 2023.

Kamanda Mhifadhi wa Nyanza za Juu Kusini wa Mamlaka hiyo alisema kijiji hicho kimekuwa ndani ya eneo la hifadhi ambapo kwa kujibu wa tangazo la serikali, wananchi wanapaswa kuwa nje ya hifadhi hiyo.

Makwati alisema zoezi litakapokamilika, wananchi wataondoka na wengine ambao wameshalipwa tayari wameanza kundoa baadhi ya mali ikiwa ni pamoja na kuezua mapaa ya majengo yao.

Mthamini Mteule wa Ardhi Mkoa wa Morogoro, Idelfonce Mtima alisema taratibu zote zimekamilika kuwezesha wananchi hao kuhama na kupisha eneo hilo.

Mtima alisema wananchi wanaofanyiwa uthamini ni 1,056 na waliohakikiwa na kustahiki kulipwa ni 807 na wengine zaidi ya 249 hawajakamilishiwa uhakiki na kwamba zoezi hilo linaendelea.

“Niwaombe tu wananchi kufuata taratibu, ambaye atakiuka taratibu za kuhama kwa siku ambazo zimepangwa atahama kwa gharama zake binafsi,” alisisitiza Mtima.

Baadhi ya wananchi waliohakikiwa na kulipwa fidia kupisha eneo la kijiji hicho kwa nyakati tofauti walishukuru serikali kwa kulipa stahiki zao kwa muda unaotakiwa na wao wamekubali kuondoka kwa hiari.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

**TANGAZO LA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA KATIKA MIKOA YA IRINGA, MBEYA NA DODOMA KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA MPWAPWA.**

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote kuwa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Awamu ya Kwanza unafanyika katika Mikoa ya Iringa, Mbeya na Dodoma katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa tarehe 27 Desemba, 2024 hadi 02 Januari, 2025. Zoezi la uboreshaji wa Daftari linafanyika kwa siku saba kwa kila kituo katika Mikoa hiyo.

1. **SIKU:** Uboreshaji unaanza siku ya Ijumaa tarehe 27 Desemba, 2024 hadi Alhamisi tarehe 02 Januari, 2025.
2. **VITUO:** Uboreshaji unafanyika katika vituo vilivyopo kwenye Mitaa, vijiji na vitongoji.
3. **MUDA:** Vituo vinafunguliwa saa 2:00 Asubuhi na kufungwa saa 12:00 Jioni.

**Uboreshaji unahusisha: -**

1. Kuandikisha Wapiga Kura wapya ambao ni raia wa Tanzania waliotimiza umri wa Miaka 18 na zaidi na hawakuwahi kuandikishwa hapo awali.
2. Kuandikisha Wapiga kura ambao watakuwa wametimiza umri wa miaka 18 siku ya tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.
3. Kuboresha taarifa za wapiga kura waliohama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine la kiuchaguzi
4. Kutoa kadi mpya kwa wapiga kura ambao kadi zao zimepotea au kuharibika.
5. Kuboresha au kurekebisha taarifa za wapiga kura.
6. Aidha,Wapiga kura wanaotaka kuboresha taarifa zao na wanaohama kituo cha kupigia kura au vyote viwili wanaweza kuanzisha mchakato wa kuboresha kwa kujaza fomu maalum kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya Tume www.inec.go.tz au anuani ya ovrs.inec.go.tz kwa kujaza namba ya kitambulisho cha Taifa, namba ya kadi ya mpiga kura, namba ya simu ya mpiga kura na jina la kata kisha watapokea ujumbe wenye namba ya utambulisho (token number) ambayo watakwenda nayo kituo cha kujiandikisha ili kukamilisha taratibu na kupata kadi ya mpiga kura.

**MAMBO YA KUZINGATIA**

- Mwananchi anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni na kusubiri hadi zamu yake ya kuandikishwa itakapowadia. Watu wenye mahitaji maalumu kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga watakaokwenda nao kituoni watapewa kipaumbele.
- Mwananchi atakapofika kituo cha kujiandikisha atachukuliwa alama za vidole vyote kumi vya mikono na kupigwa picha na kisha kupewa kadi yake mpya hapo hapo kituoni.
- Ni muhimu kujiandikisha sasa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili uweze kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na chaguzi zijazo.
- Mpiga Kura ambaye ana simu ndogo maarufu kama kitochi au kiswaswadu anaweza kuingia kwenye mfumo huo kwa kupiga *152*00#. Kisha, atachagua Namba 8 na kubonyeza, baada ya hapo atachagua namba 2 na kubonyeza, Kisha atachagua Namba 3 (Tume Huru ya Uchaguzi) na hapo, atapata huduma namba moja hadi nne. Atachagua huduma anayoitaka kati ya hizo nne. Hatimaye, atapata namba ya utambulisho (token number) atakayokwenda nayo kituoni kukamilisha mchakato wa kupata kadi ya mpiga kura.
- Mpiga kura anaweza pia kuwasiliana moja kwa moja na Maafisa wa Tume waliopo katika Kituo cha Huduma kwa Mpiga Kura kwa kupiga namba 0800112100 bila malipo.
- Zoezi hili halitawahusu wapiga kura ambao waliandikishwa awali, hawajahama maeneo yao ya kiuchaguzi na wana kadi zao za mpiga kura.

**KUJIANDIKISHA KUWA MPIGA KURA NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA**

**Limetolewa tarehe 19 Desemba, 2024 na:**

**Saida Hilal Mohammed**
**KAIMU MKURUGENZI WA UCHAGUZI**

218302902


# Asakwa kwa tuhuma za kuchoma nyumba, kuua mama na wanawe

**Na Oscar Assenga,** TANGA

JESHI la Polisi mkoani Tanga linamsaka Mwita Yoba kwa tuhuma za kuchoma nyumba na kusababisha vifo vya watu wanne; mama na watoto wake watatu.


Akizungumza jana na waandishi wa habari mjini hapa, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Almachius Mchunguzi alisema tukio hilo lilitokea Desemba 30, mwaka huu saa 4.45 alfajiri katika kitongoji cha Kwedichocho, kijiji cha Manga wilayani Handeni.

Aliwataja waliofariki kuwa ni Pili Saguge (28), mkulima na mkazi wa Kwedichocho (mama), Chacha Nyabilenga, Jane Nyabilenga na Makabala Nyabilenga.

Kamanda huyo alisema kwamba baada ya kufanya tukio hilo, mtuhumiwa alitoroka na kutokomea kusikojulikana.

Kamanda Mchunguzi alisema chanzo cha mauaji hayo ni mtuhumiwa kushtumu familia hiyo kwa madai ya kumuua mtoto wake kwa sumu, hali iliyomsukuma kutekeleza mauaji hayo kwa kulipiza kisasi.

Kamanda Mchunguzi alisema jeshi hilo linatoa wito kwa yeyote mwenye taarifa kuhusu aliko mtuhumiwa Mwita Yoba, kuwasiliana na kituo chochote cha Polisi kilicho karibu ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yake.





## Samia 'ala' mwaka mpya na watoto yatima

**Na Jaliwason Jasson,** SIMANJIRO

MSAADA wa Rais Samia Suluhu Hassan kumaliza mwaka 2024 na kuingia mpya wa 2025 kwa watoto yatima na wenye uhitaji maalum wa Kituo cha Light In Africa kilichopo mji mdogo wa Mirerani Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara umekabidhiwa kwa walengwa.

Ofisi ya Mkuu wa Wilaya hiyo, imekabidhi zawadi hizo kwenye kituo hicho kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Cuthbert Sendiga.

Kaimu Katibu Tawala (DAS) wa Wilaya hiyo, Tumaini Sebastian akiongozana na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya mji huo, Isack Mgaya, aliyasema hayo wakati wa kukabidhi zawadi hizo kwenye kituo hicho.

Tumaini, alisema zawadi hizo zilizotolewa na Rais Samia kwa kituo hicho ni mchele kilo 100, sukari kilo 25, unga ngano kilo 25, mafuta ya kula lita 20 na mbuzi wawili.

"Tunamshukuru Rais Samia kwa kuwajali watoto yatima na wenye uhitaji maalum wa kituo hiki kwa kuwapatia zawadi hizo za sikukuu," alisema.

Alitoa wito kwa watu binafsi, mashirika na taasisi kuwajali wenye uhitaji maalum na kushiriki nao kwa kuwapatia vyakula na vitu mbalimbali vya kujikimu.

Mmoja kati ya wasaidizi wa kituo hicho, Mariam Mbwambo, akizingumza wakati wa makabidhiano hayo, alimshukuru Rais Samia kwa kuwajali watoto hao na kutoa zawadi hizo kwao.

"Tunashukuru sana kwa zawadi hizi tunamuombea kwa Mungu ampe afya njema na uzima tele mama yetu na Rais wetu mpendwa Samia Suluhu Hassan," alisema Mbwambo

# Saa 72 za RC Makonda zilivyosimamisha usafiri

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

SAA 72 za Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, alizotoa kwa wageni na wakazi wa jijini hapa na viunga vyake kushiriki sherehe za kufunga na kuukaribisha mwaka 2025, zimesimamisha huduma za usafiri katika baadhi ya barabara ili kupisha shamrashamra hizo.

Makonda, alitangaza kuliteka kwa shangwe Jiji la Arusha kwa siku tatu mfululizo kuanzia Desemba 29 hadi 31, mwaka jana kwa burudani na matukio mbalimbali.

Jana Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Arusha, kilitangaza barabara zilizofungwa kupisha mkesha huo kuukaribisha mwaka mpya na kutangaza njia mbadala kwa watumiaji wa barabara ili kuepuka usumbufu.

Mkuu wa Kikosi hicho wa Mkoa huo, Zauda Mohamed alizitaja barabara zilizofungwa kuwa ni ile ya kutoka mzunguko wa jengo la Ngorongoro Tower kuelekea ofisi za Jiji la Arusha na mnara wa saa.

Nyingine ni makutano ya Barabara ya Goliondoi na Joel Maeda (maarufu Airtel) kuelekea mnara wa saa; makutano ya barabara ya Goliondoi na Uhuru (zilipo ofisi za Vodacom) kuelekea mnara wa saa.

Barabara ya makutano ya TANESCO na Fire (Zimamoto) kuelekea mnara wa saa na makutano ya Barabara ya Kanisa na Nyerere kuelekea mnara wa saa.

Kwa mujibu wa Zauda, kutokana na shangwe za kuuaga mwaka 2024, wananchi wanaotumia barabara za katikati ya jiji wanapaswa kuchagua njia mbadala.

Alisema askari wa kikosi hicho watakuwepo kutoa mwongozo wa barabara ili kupunguza msongamano.



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Muheza, mkoani Tanga, Erasto Mhina (katikati), akizungumza na vijana 20 wa kikundi cha Mishemishe kutoka Kijiji cha Mangubu, Kata ya Tongwe wilayani Muheza jana wakati wakielekea kuchangia damu katika Hospitali ya Wilaya ya Muheza ya Samia Suluhu kuukaribisha Mwaka Mpya wa 2025. Kulia ni Mganga Mkuu wa wilaya hiyo, Dk. Fani Mussa. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Same yaagizwa kutenga bajeti ya maafa

**Na Mary Mosha,** SAME

NAIBU Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, anayeshughulikia Sera, Bunge na Uratibu, Ummy Nderiananga ameiagiza Halmashauri ya Wilaya ya Same mkoani Kilimanjaro, kutenga bajeti ya kukabiliana na maafa na kuyatambua maeneo hatarishi.

Ummy alitoa agizo hilo jana wakati akikabidhi msaada wa vyakula kwa waathirika wa mafuriko ya mvua za vuli zilizonyesha usiku wa Disemba 23, mwaka jana na kuziathiri zaidi kata za Bombo, Msindo, Mtii, Maore na Vujee.

Mvua hizo zilisababisha vifo vya watu sita, uharibifu wa mazao na miundombinu ya barabara na nyumba 25.

Naibu Waziri huyo, alitembelea na kuwajulia hali waathirika wa maafa hayo na kukabidhi msaada wa mahindi tani 3.2, ndoo 25, madumu 25, vikombe na vijiko.

Alisema kutengwa kwa bajeti hiyo, kutasaidia kuwahudumia waathirika wa maafa kwa haraka pale yanapotokea, hivyo kurejeshea tabasamu wakati wanapoendelea kusubiria misaada kutoka serikali kuu.

Vilevile, aliwaagiza halmashauri hiyo kuyatambua maeneo yote hatarishi na kuanza kuwaelimisha wananchi kuchukua tahadhari ya kuhama katika maeneo hayo ili kuepuka madhara yanayoweza kutokea.

"Halmashauri sasa mna wajibu wa kuhakikisha katika bejeti yenu mnatenga fedha kwa ajili ya kukabiliana na maafa pindi yanapotokea ili muwahi mapema na kuwasaidia waathirika kwa haraka.

Lakini yako maeneo ambayo ni hatarishi maafa yamekuwa yakijirudiarudia, mnapaswa kuyatambua na kuwaelimisha wananchi wanaoishi katika maeneo hayo kuhama."


Vilevile, ameitaka Halmashauri ya Wilaya ya Same kuandaa mipango ya kukabiliana na magonjwa ya mlipuko pamoja na kuimarisha vifaa vya uokozi.

Katika hatua nyingine, amekiagiza Kitengo cha Maafa, Ofisi ya Waziri Mkuu kuhakikisha kinawapelekea wananchi hao mbegu za mahindi na mpunga haraka ili kurejesha mazao ambayo yamesombwa na mafuriko ili kuepukana kuibuka kwa janga la njaa kwa badaye.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Kasilda Mgeni, alisema katika mafuriko hayo watu 10 wamepata madhara, ambapo kati yao sita walifariki dunia kutokana na kuangukiwa na vifusi katika nyumba zao.

Kasilda, alisema nyumba 34, hekari 260 za mazao na miundombinu ya barabara, vimeharibiwa.

Alisema kwa sasa serikali inaendelea na juhudi za kurejesha mawasiliano katika maeneo hayo yalikumbwa na maafa ya mvua hizo.





# Mume ajimaliza, kisa fedha kausha damu

**Na Samson Chacha,** TARIME

MLINZI wa maduka na baa katika Mji wa Sirari, Msabi Lucas, Mkazi wa Kijiji cha Kanisani Kata ya Sirari Tarafa ya Inchugu wilayani hapa Mkoa wa Mara anadaiwa kujiua kwa kunywa sumu kwa kuibiwa Sh. 600,000 baada ya kuuza pikipiki yake.

Ndugu wa marehemu huyo, akiwemo mdogo wake, Charles Lucas alisema Desemba 29, aliuza pikipiki yake ilia pate fedha za kwenda kumlipia mke wake mkopo umiza 'kaushadamu'.

Lucas, alisema awali ndugu yao huo, alifanikiwa kumlipia madeni mengine aliyokuwa akidaiwa baada ya kuuza pikipiki hiyo alitarajia kumaliza madeni hayo.

"Alionekana kwenye baa akinywa pombe na marafiki zake na ilipofika jioni alirejea nyumbani akiwa amelewa baada ya kuzinduka alidai kuwa ameibiwa fedha zake Sh. 600,000 alizokuwa ameuza pikipiki," alisema Lucas.

Alisema ndugu na jamaa, walimshauri atulize mawazo na kufikiria alikoweka fedha hizo, badala yake alichukua maamuzi magumu ya kunywa dawa ya kupulizia mimea na kukutwa akiwa na hali mbaya.

"Mbali na kutapishwa sumu hiyo kwa kupewa maziwa na kukimbizwa hospitali lakini alifariki dunia. Tulitoa taarifa Kituo cha Polisi Sirari kwa ajili ya uchunguzi," alisema.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Sirari, Wakuru Mirumbe, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kuwaasa vijana kupunguza matumizi ya vilevi kama njia ya kuondoa msongo wa mawazo.

"Vijana ambao tunawategemea kuwa nguvu kazi wamegeukia matumizi ya pombe kali kama vile viroba, ugoro na bangi na mwenzetu isingekuwa pombe labda tungekuwa tunaonea mengine," alisema Mitumbe.

Aliwataka wananchi kuacha tabia ya kujichukulia maamuzi magumu bali wajengee utaratibu wa kufikisha malalamiko na madai yao katika vyombo husika na kupata ufumbuzi.



Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Paul Chacha (kushoto), akikabidhi zawadi mbalimbali zilizotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan kwa mmoja wa watoto wa kituo cha Mvuma kilichoko Kata ya Nyasubi, Victoria Justine, jana ili kuwapatia faraja katika sherehe ya Mwaka Mpya. Katikati ni Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita. **PICHA; SHABAN NJIA.**

# Vifo wajawazito, watoto wachanga vyapungua

**Na Elizabeth Faustine,** MAGU

VIFO vya wajawazito na watoto wachanga wilayani hapa Mkoa wa Mwanza vimepungua hadi kufikia 71 katika kipindi cha mwaka jana.

Takwimu hizo zilitolewa juzi na Kaimu Mratibu wa Elimu ya Afya kwa Umma wilayani hapa, Mussa Itembe wakati akiwasilisha mada ya afya ya uzazi wa mpango na hali ya mwenendo wa vifo kwa wazazi, wajawazito na watoto wachanga katika semina kwa madiwani na watumishi wa halmashauri iliyotolewa na Shirika la Humanity Amplify (Hao).

Itembe, alisema vifo hivyo vilitokea kuanzia Januari hadi Novemba, mwaka jana kutokana na matumizi ya dawa za kienyeji, utoaji mimba, magonjwa ya zinaa, mimba za karibu, imani potofu na mimba katika umri mdogo.

Itembe, alisema kati ya vifo hivyo vitano vya wajawazito wakati wakijifungua, 24 vya watoto wachanga, 20 wa umri wa siku sifuri mpaka saba na 22 kabla ya kujifungua.

Alisema, idadi hiyo ni ndogo ikilinganishwa na vifo 88 vilivyotokea mwaka juzi.

Alisema idadi kubwa zaidi ya vifo hivyo 120 vilitokea mwaka 2021/2022.

Itembe, alisema halmashauri hiyo inafanya jitihada kupunguza vifo hivyo, ikiwamo kutoa elimu kwa jamii na kuhamasisha matumizi ya uzazi wa mpango.

Alisema kutokana na jitihada hizo, wanatarajia mabadiliko mwakani baada ya kufikisha elimu ya uzazi wa mpango na kuboresha huduma za kujifungua kwenye kliniki na vituo vya afya.

Ofisa Ustawi wa Halmashauri hiyo, Maryciana Mayengela, alisema wahudumu wa afya wanaendelea kutoa elimu ya madhara ya kutumia dawa za kienyeji kuharakisha uchungu kwa wajawazito kwa kusababisha vifo wakati wa kujifungua.

Marciana, alitoa wito kwa jamii hususani wajawazito kuepuka dawa hizo wanapohisi uchungu badala yake wawahi kliniki na kwenye vituo vya afya kupata huduma sahihi.

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Mohamed Ramadhani, aliwataka washiriki wa semina hiyo kutoa elimu hiyo kwa jamii na kuhamasisha matumizi ya uzazi wa mpango na wajawazito na wenza wao kuhudhuria kliniki kutokana na mwitikio kuwa mdogo.

Ofisa Tathmini na Takwimu wa shirika hilo, Restute Jacob, alisema wameanza kutoa semina hiyo ili upunguza vifo vitokanavyo na uzazi, mimba za utotoni na wasichana kuachishwa shule waozeshwe.

"Tumekubaliana kuweka mpango mkakati na madiwani kwenda kutoa elimu kuhusu madhara ya ndoa hizi na kuwaelimisha wananchi umuhimu wa kufichua ukatili wa kijinsia," alisema Restute

# Mwalimu matatani kwa kubaka mwanafunzi maktaba

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

JESHI la Polisi Mkoa wa Mwanza linamshikilia mwalimu wa kujitolea katika Shule ya Msingi Nyangh'omango iliyopo wilayani Misungwi kwa tuhuma za kumbaka mwanafunzi mwenye umri wa miaka 13 wakati akijisomea maktaba.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa huo, Willbroad Mutafugwa, alithibitisha kukamatwa kwa mwalimu huyo juzi jijini hapa.

Mutafugwa, alisema tukio hilo lilitokea Desemba 23, mwaka jana majira ya saa 12 jioni baada ya mwanafunzi huo kwenda kujisomea katika chumba cha maktaba ya shule hiyo.

Alisema wanaendelea kufanya uchunguzi wa tukio na kwamba mtuhumiwa huyo atafikishwa mahakamani hivi karibuni.

# Kijana mbaroni kwa kumuua babu yake

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

CHARLES Hindya (19), Mkazi wa Kijiji cha Mwasengela wilayani Misungwi Mkoa wa Mwanza ametiwa mbaroni kwa tuhuma za kumuua babu yake Charles Makula (62) kumpiga na kitu butu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Wilbrod Mutafungwa, tukio hilo lilitokea Desemba 24, mwaka jana, majira ya saa 11 jioni.

"Chanzo cha mauaji hayo ni mtuhumiwa huyo kuugua ugonjwa wa akili," alisema.

Akizungumzia tukio jingine, Kamanda huyo, alisema wanamshikilia Fundi Magari, Novatus Mtesingwa (34), Mkazi Nyasaka kwa tuhuma za kumuua mwenzake, Ibrahim Zacharia (28) kwa kumpiga kwa kitu chenye ncha kali kichwani kutokana na wivu wa mapenzi

Alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa akiwa mafichoni mkoani Dodoma alipokimbilia baada ya kumuua Zacharia ambaye ni fundi mwenzie.

Mutafugwa, alisema mwili wa marehemu huyo ulipatikana Desemba 28, mwaka huu majira ya saa 4 asubuhi eneo la Lukobe Kahama wilayani Ilemela.

Alisema chanzo cha mauaji hao ni wivu wa kimapenzi.

Katika tukio jingine; polisi wanamshikilia Paschal Kiliyaya (24), Mkazi wa Isamilo wilayani Sengerema kwa tuhuma za kukutwa na ng'ombe 28 za wizi mali ya John Swalala (61).

Kwa mujibu wa Mtafungwa, mtuhumiwa anaendelea kuhojiwa na atafikishwa mahakamani kujibu mashtaka.

Ukurasa 14



**2024 IMETESA WENGI**
**TRUMP APIGWA SHABA, GEN Z IKIMTIKISA RUTO, GACHAGUA 'OUT', KINDIKI AKIMRITHI**

Ukurasa 12



**Hivi ndivyo watu wasiojulikana walivyotikisa nchi mwaka 2024**



# Karibu mwaka mpya utujibu CHADEMA ya Mbowe au Lissu

**Na Restuta James**

ZIKIWA zimesalia siku 20 kufikia uchaguzi wa viongozi wa kitaifa wa CHADEMA, mwenyekiti Freeman Mbowe na Makamu Tundu Lissu, anayetaka kumrithi, agenda zao kuu ni tatu.

Kudai katiba mpya, mifumo huru ya uchaguzi na sheria rafiki za kusimamia uchaguzi, ndiyo madai yanayobebwa na Mwenyekiti Taifa, Mbowe na Makamu Lissu.

Wote wamebeba agenda hizo lakini kila mmoja ana mipango ya namna ya kuyadai kwa watawala.

Lissu anayetaka kuwa bosi namba moja kutoka namba mbili aliko hivi sasa, haamini sana katika maridhiano bali anategemea kuona agenda hizo zinapata majibu kwa njia anayoeleza ni ya mazingira ya sasa ya kisiasa.

Mbali na mambo hayo matatu, Lissu anataka aifumue katiba ya CHADEMA ili kuweka kikomo cha uongozi ndani ya chama na ule wa ubunge wa viti maalum na udiwani.

Anasema anataka aanze kufanya mabadiliko kuanzia ndani ya chama kwenye mifumo ya uchaguzi, ili madai ya uchaguzi huru wa nchi yawe na tija zaidi.

"Kipindi cha siasa ngumu kinahitaji watu wagumu. Wanaoweza kusimama hadharani wakasema maneno yanayostahili. Wenye msimamo wa kuaminika, uadilifu usiokuwa na shaka. Huu ni muda sahihi kwangu kugombea nafasi ya Mwenyekiti," anasema Lissu.

Msimamo wa Lissu kutoamini katika maridhiano ni kile anachosema kwamba CCM, kwa upande mmoja na serikali kwa upande mwingine, hawako tayari kupata muafaka wa kitaifa kwa kile anachoona, mifumo na katiba iliyopo inakinufaisha zaidi chama hicho.



Tundu Lissu, mpinzani wa Mwenyekiti Freeman Mbowe, kwenye uchaguzi mkuu baadaye mwezi huu. **PICHA: MTANDAO**

Hiyo ndiyo sababu inayomfanya tangu mwanzo, kupinga mazungumzo ya maridhiano kati ya CHADEMA, CCM na serikali, anasema Lissu.

"Nilimpinga Mbowe, kwenye maridhiano na baadaye akasema mwenyewe wenzake waliompinga, walikuwa sahihi. Tungeimba wote wimbo wa maridhiano, tungekuwa wapi leo. Tuwe na ujasiri wa kusema hii haiko sawa hata kama inasemwa na wakubwa zetu," anasisitiza.

**MWENYEKITI MBOWE**

Anaamini katika maridhiano na kwamba njia hiyo itasaidia kuunganisha makundi yote katika jamii.

Hata hivyo, anatofautiana na Lissu kuhusu marekebisho ya katiba ya CHADEMA ili iendane na mazingira ya sasa, akieleza kuwa hilo linaweza kujadiliwa ndani ya vikao vya chama na si kwenye majukwaa ya kisiasa.

Mbowe anasema ili hoja tatu kuu za chama hicho zipate muafaka wa kitaifa, zinahitaji ushirikiano wa wanasiasa, asasi za kiraia, wanazuoni, viongozi wa dini, wasomi na mwananchi mmoja mmoja.

Msimamo wake anauweka kwa kauli yake alipokwenda kuchukua fomu akisema:

"Tunahitaji katiba kwa kucheza miguu yote, ya diplomasia, ushirikishwaji, barabara na kila silaha itumike. Na hii ni ajenda ya msingi katika chama chetu."

Katika kujenga msingi wa msimamo wake, ananukuu kauli 10 za viongozi mashuhuri duniani, akiwamo Hayati Nelson Mandela aliyekuwa mpigania uhuru na rais wa Afrika Kusini, Makatibu Wakuu wastaafu wa Umoja wa Mataifa, Ban Ki-Moon na Koffi Anan, marais wa Marekani, Jonh Kennedy na Barack Obama, Kansela mstaafu wa Ujerumani, Angela Markel, Waziri Mkuu wa zamani wa Uingereza Winston Churchil na Waziri Mkuu wa India, Mahatma Gandhi, ambao kwa nyakati mbalimbali walihimiza umuhimu wa meza ya maridhiano hasa kunapotokea tofauti kubwa za kisiasa.

Raia hao wa dunia, walinukuliwa kwa nyakati tofauti wakieleza kuwa mazungumzo yanafanywa na watu jasiri walio tayari kupoteza kidogo ili wapate kikubwa chenye maslahi ya umma.

Anaona kwamba licha ya mazungumzo kati ya CHADEMA na CCM kukwama, chama hicho kikuu cha upinzani kilipata mafanikio makubwa ikiwamo kufunguliwa kwa mikutano iliyokiwezesha kusajili wanachama nchi nzima, kufanya uchaguzi wa ngazi zote na kufutwa kwa kesi zaidi ya 400 zilizokuwa zimebambikiwa kwa viongozi na makada wake, maeneo mbalimbali, kurejea nchini kwa viongozi waliokuwa wamekimbilia ughaibuni na kulipwa haki yao ya ruzuku ya chama iliyokuwa imezuiwa kwa miaka miwili.

Anaamini kwamba hata sasa, chama hicho kimefanikiwa kufanya uchaguzi katika ngazi mbalimbali, kutokana na maridhiano, ambayo yalifanikisha kufuta katazo haramu la miaka saba la kuzuia mikutano ya vyama vya siasa.

"Maridhiano si jambo jepesi, lakini ni kitu kisichoepukika kwenye siasa duniani kote. Makundi mbalimbali yanachukua upande wa maridhiano kutokana kile inachotamani," anasema.

"Ninajivunia sana mazungumzo na uamuzi wetu wa kuingia kwenye maridhiano."

**KURA MITANDAONI**

Wakati viongozi hao wakichuana, hali ni hiyo hiyo mitandaoni kila upande ukieleza sababu za kumuunga Lissu au Mbowe mkono.

Kwenye jukwaa la Jamii Forums, Lissu anaongoza kwa asilimia 83.3 ya kura zilizoanza kupigwa wiki iliyopita huku Mbowe akiwa na asilimia 16.7. upigaji wa kura hizo utahitimishwa Jumatatu ijayo.

Hata hivyo, maamuzi rasmi ya nani atakiongoza chama hicho yatafanywa na wajumbe 1,200 wa mkutano mkuu wa CHADEMA.

"Lissu anapendwa na wapiga kura na hili ndilo lengo la chama cha siasa. Mbowe anaweza kupendwa na wajumbe wa Mkutano Mkuu lakini bila wananchi, chama ni mufilisi. Kitabaki tu kuwa chama cha kuitwa Ikulu kunywa chai na kupiga picha," anaeleza mmoja wa wachangiaji kwenye ukurasa wa kura za maoni kwenye jukwaa la Jamii Forums.

Msimamo wa CHADEMA ni 'no reforms, no election' na ndiyo inayowafanya Mbowe na Lissu kuzibeba agenda tatu za chama hicho.

# Hivi ndivyo watu wasiojulikana walivyotikisa nchi mwaka 2024

NA MWANDISHI WETU

MWAKA 2024 umefika tamati jana saa 5:59 usiku. Leo ni siku mpya na mwanzo wa mwaka 2025. Heri na hongereni wasomaji wa Nipashe na wapenzi wa Kijarida cha Siasa.

Kama ilivyo miaka mingine iliyopita, 2024 ulijaa milima, mabonde, tambarare. Yaani kila aina ya matukio yakiwamo ya kufurahisha na pia kusikitisha ambayo huenda yamelitia taifa doa .

Katika mwaka huo wa 2024, kuliibuka matukio ya kuteka watu wakiwamo wafuasi wa vyama vya siasa katika mazingira ya kutatanisha na kuzua hofu na taharuki miongoni mwa Watanzania.

Utekaji watu huo uliwaibua wanasiasa, wanaharakati na wadau wa haki za binadamu na kupaza sauti wakitaka waliotekwa au kukamatwa na watu wasiojulikana wawaachie huru waseme walipowaficha.

Hata hivyo, juhudi hizo hazikuzaa matunda kutokana na kile ambacho kimekuwa kikielezwa na baadhi ya wanasiasa kuwa wafuasi wao wametekwa na hadi sasa hawajulikani walipo.

Wapo ambao walidai kutekwa lakini baadaye wakapatikana wakiwa hai ingawa inaelezwa kuwa walikuwa wameumizwa katika sehemu mbalimbali ya miili yao.

Mtindo wa kuteka ulishuhudiwa na baadhi ya wakazi wa Kiluvya Dar es Salaam wakati mtu mmoja akitaka kutekwa, lakini bahati nzuri akawazidi nguvu watekaji wakashindwa kumuingiza katika gari.

Tukio hilo lilitokea Novemba mwaka huo wa 2024, lakini kutokana na ukubwa wa mwili na uzito wa mtekwaji vilisababisha watekaji kushindwa kumwingiza katika gari waliokuwa wakiitumia.

Video ilirushwa katika mitandao akisikika akiomba msaada kwamba anakwenda kuuawa, akitaka wamsaidie, lakini watu waliokuwapo eneo la tukio walikuwa wakitazama bila kutoa msaada.

"Nisaidieni naenda kuuawa, naenda kuuawa, siwajui hawa, naenda kuuawa" alipambanania uhai hadi akafanikiwa kuwashinda huku wakimwachia pingu ambazo walikuwa tayari wamemfunga.

Kwa mwaka huo wapo waliodai kutekwa na kubahatika kupatikana akiwamo Abdul Dondo ambaye ni kiongozi wa Ngome ya Vijana ya Chama cha ACT Wazalendo.

Juni 23 mwaka huu, Edgar Mwakabela 'Stiva' alitekwa jijini Dar es Salaam, lakini baadaye akapatikana akiwa ametupwa katika msitu mkoani Katavi akiwa na majeraha.

Wengine wanaodaiwa kutekwa na watu wasiojulikana na hadi sasa hawajapatikana ni mwenyekiti wa CHADEMA wilaya Temeke, Deusdedith Soka na kabu wake Jacob Mlay.

Septemba 6 mwaka huu, mwanachama wa CHADEMA, Ally Mohamed Kibao alitekwa na watu wasiojulikana eneo la Tegeta Dar es Salaam, kisha siku iliofuata mwili wake ukaokotwa akiwa ameuawa.



Katibu Mwenezi wa Baraza la Wanawake CHADEMA Taifa, Aisha Machano, alidai kutekwa, kuumizwa na kutupwa porini. **PICHA: MTANDAO**

**TAKWIMU ZA TLS**

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), ikirejea utafiti wake, Wakili Boniface Mwabukusi, watu 83 wanaodaiwa kutekwa au kupotea kwa miaka minane kuanzia mwaka 2016 hadi 2024.

Taarifa hiyo ya TLS iliyotolewa kwa vyombo vya habari mwaka jana, inaonyesha wazi kuwa mambo ya kuteka watu yameendelea kujitokeza kila mwaka na inawataja baadhi ya waliotekwa.

Miongoni mwa wanaotajwa na Rais wa TLS na majina ya mikoa yao kwenye mabano ni Ben Saanane (Dar), Azory Gwanda (Pwani), Simon Kanguye (Kigoma) na Joshua (Iringa), Kombo Twaha (Handeni-Tanga), Kennedy Mwamlima (Mbeya), Edger Mwakalebela (Dar), James Sije (Nyakato-Mwanza), Joseph Mnyonga (Mwanza), Dotto Kabwa (Ifunga-Iringa) na Yahya Ally (Dar).

Rais huyo anawataja wengine kuwa Chande Kizega (Dar), Mzee Samuel Mkongo (Geita Mjini), Charles Mwampyate (Dar), William Herman (Kangaye-Mwanza), David Lema (Mwanza), Jerome Kisoka (Kilimanjaro) na Ridhiwani Msangi (Iringa).

Katika kundi hilo, wamo pia Benson Ishungisa (Dar), Hamza Said (Mwatulole-Geita), Yonzo Dutu (Kishapu-Shinyanga), Lilenga Isaya (Mwandiga-Kigoma), Tawafiq Mohamed (Dar), Self Swala (Dar), Edwin Kunambi (Dar), Hemed Abass (Dar) na Maseke Mwita (Mara)

Aidha, wamo pia Rajab Mdoe (Dar), Mzee Haji Soft (Dar), Alphonce Bilasenge (Kagera), Albert Selembo na Moloimeti Saing'eu, Ndirango lazier, Joel Lessonu, Simoni Orosikiria na Damian Laizer.

Katika mchanganyiko huo wa miaka ya nyuma na 2024, anawataja pia Taleng'o Leshoko, Kijoolu Olojiloji, Shengena Killeli, Malongo Paschal, Simeli Korongoi, Ingoi Kanjwei, Sangau Ngiminis, Marijoi Parmati, Morongeti Masako, Kambatai Lulu na Orias Oleng'iyo na Luacs Njausi, hata hivyo mikoa yao haikutajwa.

Anaendelea kuwataja wengine kuwa ni Matthew Siloma, Wilson Kolong, James Taki, Joseph Jartan, Kelvin Nairoti, Lekerenga Orodo, Fred Ledidi, Simon Morintanti wote kutoka Loliondo, mkoani Arusha.

Vilevile wamo Mohamed Kalebe (Geita), Amon Magige (Mwanza), Aziz Kinyonga na Yusuph Dudu (Dar) Kastory Kapinga (Mbinga), Dioniz Kipanya (Rukwa), Shadrack Chaula (Mbeya) na Prosiper Mnjari (Dar).

Wengine ni Thomas Ihuya (Mwanza), Dennis Kantanga (Shinyanga), Damas Bulimbe na Lucas Bulimbe (Geita), Matuki Makuru (Mara), Dastan Nestory na Adinan Mbezi wote kutoka Geita.

Katika msururu huo wamo Lengaripo Lukumay (Mwanza), Akidu Salim (Dar), Enock Chambala (Tanga), Dioniz Kipanya (Katavi), Nusra Omari (Dar), Theresphora Mwakalinga (Dodoma), Donald Mboya (Kagera), Ilham Makoye, Barack Majigeh, Yusra Musa, Angel Kamugisha, Brighton Emmanuel wote wa Dar.

Taifa kama dunia limeingia mwaka mwingine wa 2025, ambao nuru ns mwelekeo wa Watanzania wengi wanatamani uwe wa amani na utulivu.

***HERI YA MWAKA MPYA 2025***

# 2025 kujibu maana ya demokrasia, kufungua dira mpya ya maendeleo

**NA GAUDENSIA MNGUMI**



Dira na demokrasia ni muhimili kwa ustawi wa taifa linalothamini usawa wa kijinsia. **PICHA: MTANDAO**

KARIBU mwaka mpya 2025. Wasomaji na wapenzi wa Kijarida cha Siasa cha Nipashe pokeeni maua yenu na heri nyingi.

Ni mwaka wa jambo letu yaani uchaguzi wa marais wa Tanzania na Zanzibar, wabunge, wawakilishi na madiwani.

Lakini kwanza itakapofika Juni utakuwa mwanzo mpya kwa Tanzania baada ya kuzindua na kuanza kutekeleza Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2050. Inaanza kutumika baada ya ile ya 2025 kumaliza muda wake.

Taifa lenye demokrasia ya kweli ni lazima liwe na dira ambayo ni malengo ya kufikiwa au maono ya mbali ya kutaka lifike huko kwa kipindi fulani.

Dira hiyo huonekana katika mipango, mifumo inayoandaliwa, sheria, taratibu, miongozo na mikakati mbalimbali ya kujenga uchumi na jamii imara inayolingana na wakati unaotazamwa.

Serikali imeandaa malengo au dira na kwa kuona kuwa ni lazima watu wenyewe wapange na kukubaliana na kile wanachotaka na namna ya kufikia lengo ya maono hayo. Dira 2050 imewashirikisha watu katika kuiandaa kadhalika ndiyo muhimili katika kuitekeleza.

Kwa hili la dira serikali imedhihirisha umuhimu wa demokrasia shirikishi kwa kupokea maoni ushauri na fikra kutoka karibu kila kundi ili kuwa na dira inayobeba maoni na mitazamo ya Watanzania wote.

Mwaka 2025 ni wa umuhimu wa kipekee mbali na dira umebeba jambo muhimu, ndiyo msimu wa uchaguzi mkuu wa marais wa Jamhuri ya Muungano na Zanzibar, wabunge, wawakilishi na madiwani. Unafanyika wakati Tanzania ikitimiza miaka 33 ndani ya mageuzi ya kisiasa.

Zama hizi mageuzi hayo ya kisiasa yameboreshwa zaidi na falsafa ya Rais Samia Suluhu Hassan ya R4 zenye maudhui ya "Reconciliation" au maridhiano au kupatana kwa makundi yote yanayohasimiana, "Resilience" yaani ustahimilivu, Reforms" kwa maana ya mageuzi na kuzungumzia mabadiliko ili kuwa na kesho iliyo bora zaidi na "Rebuild" ikimaanisha kujenga taifa upya.

Rais anakuja na falsafa hiyo kwa sababu licha ya kuwa na mfumo wa vyama vingi, kulikuwa na mkwamo wa kisiasa ambao ulivifungia vyama vingine vya kisiasa kushiriki kwenye masuala ya kidemokrasia katika awamu ya tano, suala lililorejesha nyuma na kuzifungia milango ya harakati za kuendeleza demokrasia vyama vya upinzani, taasisi za kiraia na ya kubinya uhuru wa vyombo vya habari.

Mwaka 2025 unapoanza na ajenda ya uchaguzi, la muhimu kuzingatia ni kwamba mfumo wa vyama vingi ni mageuzi ya kisiasa kutoka katika serikali yenye chama kimoja na kuingia kwenye vyama vingi.

Huku ndiko kuwa na wigo mpana wa demokrasia. Mara kadhaa tafsiri ya demokrasia imetolewa na kuna umuhimu wa kuikumbusha tena kuwa ni neno la Kigiriki.

'Demos' kwa maana ya watu na 'Kratos au cratos' ni uwezo au nguvu ama mamlaka. Hivyo humaanisha uwezo wa raia kujitawala wenyewe kwa manufaa yao.

Utawala wa raia wenyewe huwakilishwa na watu wenyewe lakini kwa njia tofauti kwa mfano kupitia mikutano ya hadhara na mijadala ndiyo maana R4 ya maridhiano na ile ya uhimilivu zinafungua milango ya mikutano ya wanasiasa wapinzani pamoja na harakati zote za kisiasa katika kutoa ya moyoni, kukosoa, kuelekeza ili kuboresha..

Kadhalika, kuna kutoa maoni mfano kwenye mitandao ya kijamii, vyombo mbalimbali vya habari, kwenye mijadala, mihadhara vyote vikitumiwa kutoa maoni ya watu kwa ajili ya faida ya kukomaza demokrasia na kuleta ustawi.

Watu wanaoweza pia kuchagua wawakilishi ndiyo maana ya uchaguzi mkuu wa mwaka huu wa 2025 na pia wananchi wanakuwa na taasisi zao za kirai , ndizo AZAKI zinazojumuisha wadau, sekta na makundi mbalimbali kuzungumzia maoni na ushauri wao.

Sharti kubwa la demokrasia ni hili, hakuna kujilimbikizia madaraka bali kugawanya madaraka na kuwa na uwakilishi na ushiriki mpana unaogusa karibu kila mtu na kuwapo na taasisi mbalimbali zikifanyakazi tofauti na pia zikitumiwa kufanya 'checks and balance'.

Katika mgawanyo huo wa madaraka kuna bunge , baraza la wawakilishi ndiyo wawakilishi wa wananchi, watunga sheria, wachambuzi na wapitisha bajeti na wasimamizi wa serikali.

Iko serikali hapa ndipo kuna viongozi kuanzia rais, baraza la mawaziri, makatibu wakuu, watendaji wakuu, maofisa, mameneja na wakuu wa vitengo, vyombo na idara za umma zinazofanyakazi kwa ajili ya wananchi. Hawa wanafanya maamuzi na kusimamia utendaji kazi wa kila siku uwe wa kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Upo muhimili wa sheria ni mahakama, ndani yake kuna majaji, mahakimu, wapo mawakili ambao ni walinzi wa sheria na katiba, waamuzi wa kesi za jinai na madai na kwa ujumla kutafsiri sheria na kusimamia haki.

Pamoja na hayo kuna taasisi nyingine za kuendelea kufuatilia mfano AZAKI, vyombo vya habari navyo ni jicho muhimu kwenye kuendeleza demokrasia.

**SIFA ZA DEMOKRASIA**

Kikubwa ni uchaguzi huru, halali, wa haki na unaokubalika. Taifa linapoingia 2025 ambo ni mwaka wa uchaguzi wanasiasa wakumbuke kuwa demokrasia ya kweli huonekana wakati wa uchaguzi.

Ni mchakato unaoanza na jinsi wagombea wanavyoteuliwa na vyama vyao, walivyopigiwa kura na kupitishwa, kura zilivyopigwa vituoni, zilivyohesabiwa na kutangazwa matokeo au mshindi.

**UTAWALA KISHERIA**

Kwenye demokrasia kanuni hii inasimama kwamba, sheria ni kipimo cha mwenendo wa taifa na raia na ili demokrasia iwepo ni lazima sheria zake ziwe za kuendeleza maisha ya watu wote na kuleta usawa katika jamii hasa kwenye kupata na kutumia huduma muhimu na za lazima na pale inapoonekana kuna upungufu ikibidi zibadilike kila wakati kulinda haki , ustawi na maendeleo ya raia.

**UHURU KIFIKRA**

Serikali yenye demokrasia ya kweli, watu wake wana uhuru wa fikra na kutoa maoni au mawazo bila kuogopa au kutishwa na utawala. Fikra na mawazo yao ni kwa faida yao na taifa pia.

Watu wawe na uhuru wa kuandika habari kuhusu maisha yao, changamoto, fursa bila kuogopa na wakati mwingine ni lazima kukubali upinzani kama Rais Samia anavyosema kuwa ni lazima kuukubali upinzani kwa ajili ya kujenga maana ni muhimu katika nchi.

Wakati huu kuelekea kwenye uchaguzi mkuu lazima serikali ilinde uhuru wa watu wake si kuuingilia. Uchaguzi ili uwe huru ni lazima watu walindwe si kutishiwa maana hatua kama hizo zinaleta woga na kunyong'oneza demokrasia.

***HERI YA MWAKA MPYA 2025***

## 2024 IMETESA WENGI

# Trump apigwa shaba, Gen Z ikimtikisa Ruto, Gachagua 'out', Kindiki akimrithi



Rais mteule wa Marekani, amepona sikio akitarajia kuingia ikulu Januari 20 . **PICHA ZOTE MTANDAO**



Kithure Kindiki Naibu Rais wa Kenya baada ya mapinduzi ya GEN Z .

**Na Christina Mwakangale**

ZIMEBAKIA siku 19 mbabe Donald Trump, arudi tena ndani ya ikulu ya Marekani ya White House, baada ya kuchaguliwa kwa kishindo.

Anarejea baada ya kumshinda mpinzani wake Makamu wa Rais wa sasa mwanamama Kamala Harris wa chama cha Democrat.

Trump mwenye miaka 78 hatausahau mwaka jana kwa vile wakati wa kampeni wababe walitaka kumaliza maisha yake, kwa kumpiga risasi tena iliyolenga kichwani ikitua sikioni, mkasa ukitokea mwezi Julai.

Akiwa kwenye kampeni ndania ya jimbo la Pennsylvania wakati akihutubia, milio ya risasi ilisikika kwenye mkutano wa hadhara.

Alinusuriwa kwenye jaribio hilo na maofisa usalama akiamini mhusika aliazimia kumuua, baada ya kurushiwa risasi sikioni. Katika chapisho lake kwenye mtandao wake wa Truth Social anasema.

"Risasi ilipenya sehemu ya juu ya sikio la kulia."

Mtuhumiwa alipigwa risasi na kufa papo hapo katika eneo la tukio na maofisa wa secret service au wana usalama.

Wakati mwaka 2024 unemalizika, barani Afrika, wapo wanasiasa kadhaa waliotikiswa ndani ya mamalaka.

Ni jirani Kenya, Rais William Ruto, akikimbizwa mchakamchaka na maandamano ya miezi kadhaa, yaliyopewa jina maarufu Gen Z au Generation Zero, kwa maana kizazi cha mwishoni mwa karne 21, yakimtikisa.

Akichukua maamuzi kadhaa ikiwamo kubadilisha baadhi ya viongozi wanaomzunguka akianza na makamu wake Rigathi Gachagua.

Naibu Rais anatuhumiwa kumhujumu Rais Ruto, kufadhili na kuhamasisha GEN Z kuvuruga serikali.

Aidha, analichambua baraza lake la mawaziri na kuwatumbua baadhi huku akiingiza wapya. Gachagua mwenyewe akidai kuwa ametolewa kafara' chanzo kikianzia kwenye maandamano hayo.

Vijana wa Gen Z hoja yao ya kuingia mtaani na hata kidiriki kulivamia bunge, kujipiga picha za simu maarufu -selfie wakishikilia siwa, ni pamoja na madai kuwa maisha yamekuwa ghali chini ya uongozi wa Ruto.

Mara kadhaa Ruto anadai ndani ya maandamano hayo kuna uratibu wa kisiasa na hayana uhalisia wa akitoa lawama kwa viongozi tofauti waliokwisha staafu.

Kenya inashuhudia machafuko ya wiki tatu mfululizo waandamanaji wakivamia bunge Juni 25 baada ya muswada wa fedha uliopendekeza nyongeza ya kodi kupitishwa.

Muswada huo uliwakera ni baada ya kuwaongezea kodi Wakenya licha ya kodi ya nyumba ya asilimia 1.5 iliyowekwa awali na ile ya bima ya matibabu ya asilimia 2.7.

Kwa mujibu wa mashirika ya kutetea haki za binadamu, zaidi ya watu 41 wameuawa katika maandamano hayo, ambayo yalibadilika na kuwa wito wa kumtaka rais kujiuzulu.

Uvamizi huo wa bunge ambao ni wa kwanza katika historia ya Kenya, unasababisha uharibifu mkubwa lakini ukiwashangaza wengi sio tu Afrika na duniani

**GACHAGUA ARITHIWA**

Baada ya vuta nikuvute Bunge la Taifa la Kenya likapitisha jina la mrithi wa naibu wa rais, Kithure Kindiki, na kumweka pembeni Gachagua kwa kura ya kutokuwa na imani naye.

Alikuwa Waziri wa usalama wa taifa na alichukua nafasi hiyo baada ya bunge kupiga kura kumpa ridhaa.

Katiba ya Kenya inaelekeza kuwa baada ya jina la mrithi wa naibu kuwasilishwa na rais, bunge la taifa lina lazima kumridhia au kumkataa, kazi iliyofanyika Oktoba mwaka huu.

**WALIA NA UTAJIRI**

Utajiri wa ghafla wa baadhi ya viongozi umewastua baadhi ya Wakenya likiwamo Baraza la Wazee nchini humo.

Kwa ujumla liliwaunga mkono vijana na maandamano ya Gen Z likimtaka Rais Ruto, kukabiliana na ufisadi uliokithiri katika serikali yake.

Wazee hao wanaomba uwajibikaji katika serikali wakitaka kujua jinsi baadhi ya viongozi walivyo matajiri ghafla na kutangaza utajiri wao hadharani.

"Tumeona watu waliokaa madarakani kwa muda usiozidi miaka miwili wakiwa na mamilioni ya fedha, wakitumia ndege kusafiri kutoka eneo moja hadi jingine mbali na kutoa michango ya mamilioni ya hela kila wikendi katika harambee bila kujali vijana ambao hawana ajira," ni moja ya madai yao.

**MOTO KOREA**

Mustakabali wa Rais wa Korea Kusini, Yoon Suk Yeol, umebakia njia panda, baada ya usiku wa machafuko.

Ni hatua inayokuja baada ya kutangaza sheria ya kijeshi na kisha kuiondoa ghafla na kuitumbukiza nchi hiyo katika machafuko.

Yoon, ambaye alishinda urais kwa kura chache 2022, hakupendwa sana na Wakorea Kusini na amekuwa akikabiliwa na shinikizo tangu ashindwe uchaguzi wa bunge Aprili, mwaka huu.

Hatua hiyo aliyochukua inaonekana kuwa sawa na kura ya kutokuwa na imani naye.

Pia amekumbwa na matatizo binafsi, akiomba msamaha katika hotuba yake kwa taifa kwa msururu wa mabishano yaliyomhusu mkewe ambayo ni pamoja na madai ya kukubali mkoba wa kifahari zawadi kutoka kampuni ya vitu vya kifahari ya Dior ya Ufaransa na udanganyifu wa uwekezaji wa hisa.

Bunge la Korea Kusini limepiga kura kumuondoa madarakani Rais Yoon Suk Yeol, kutokana na jaribio lake lililoshindwa la kutangaza sheria ya kijeshi iliyodumu kwa muda mfupi. Lilipiga kura Desemba 14, 2024, kumuondoa madarakani rais huyo.

Kati ya wabunge 300, 204 wamepiga kura ya kumuondoa rais madarakani kwa madai ya uasi, huku 85 wakipiga kura ya kupinga. Watatu hawakupiga kura, huku kura nane zikibatilishwa.

***MITANDAO***

***HERI YA MWAKA MPYA 2025***





## Wananchi watakiwa kutunza miundombinu ya barabara

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

BARAZA Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Wilaya ya Dodoma mkoani hapa, limewataka wananchi kutotumia sherehe za mwaka mpya wa 2025 kujihusisha na vitendo viovu vya uharibifu wa miundombinu.

Mwenyekiti wa BAKWATA wa Wilaya hiyo, Bashiru Hussen alitoa rai hiyo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa.

Hussein, alisema badala ya kujihusisha na vitendo hivyo watumie muda huo kumshukuru Mungu na kuliombea Taifa amani na utulivu uliopo ili liendelee kuwa na maendeleo kiuchumi.

Alionya kuwa vitendo vya uvunjifu wa amani vinavyofanywa wakati wa kusheherekea sikukuu hiyo, vimekuwa vikiigharimu serikali na jamii kutokana na uharibifu wa miundombinu hiyo.

Aliwaomba viongozi wa dini kutumia nyumba zao za ibada kuwahamasisha waumini kuungana kwa ajili ya kufanya dua na sala.

Kadhalika, Hussein, aliwataka wazazi na walezi kutowasahau watoto wao wanaosoma kwa kuwaandalia vifaa vya shule ili kuepukana na changamoto za kushindwa kuripoti kwa wakati.

"Pamoja na maandalizi yote hayo ya mwaka mpya ninawaomba wazazi na walezi kutowasahau watoto vifaa vinavyohitaji shuleni,"alisema

# Mbunge kuiomba serikali kutenga siku kwa makundi ya WhatsApp

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MBUNGE wa Iramba Mashariki, Francis Mtinga amesema atawasilisha hoja binafsi bungeni kuiomba serikali iweke siku maalum ya makundi ya wanachama wa mitandao ya kijamii ya WhatsApp kufanya mambo yao na shughuli za maendeleo kwa jamii.

Mtinga alitangaza mpango wake huo juzi kwa wanafunzi waliosoma Shule ya Sekondari Mwenge iliyopo Manispaa ya Singida ambao wapo katika kundi moja la whatsApp kutoka mikoa mbalimbali nchini baada ya kukutana na kufanya kazi ya kupanda miti katika shule hiyo.

Mtinga, alisema makundi hayo ya whatsApp yanawakusanya watu mbalimbali na baadhi yamekuwa na manufaa makubwa kwa jamii kutokana na kushiriki shughuli mbalimbali za maendeleo na kusaidiana.

Alisema hivyo kuna umuhimu wa kutenga siku maalum itambulike kisheria kwa ajili ya shughuli hiyo.

Alisema suala hilo ambalo anaamini ataungwa mkono na wabunge wenzake, makundi ya whatsapp yatakapokuwa yametambulika rasmi kisheria hata taasisi, mashirika na kampuni yatakuwa yanawaruhusu wafanyakazi wao kwenda kushiriki shughuli itakayokuwa imeandaliwa na kundi lao.

"Baadhi ya wanachama wa makundi ya mitandao ya kijamii ya WhatsApp wanapokuwa wana jambo lao la kwenda kufanya nje, mfano ya kituo cha kazi inakuwa vigumu kwenda kwa bosi wake kuomba ruhusa kwasababu suala la group la whatsApp halitambuliki," alisema.

Mtinga aliwaomba wabunge wenzake siku atakapowasilisha hoja bungeni aungwe mkono ili serikali ikubali kutenga siku maalum ya makundi hayo.

Makundi ya mitandao ya kijamii ya WhatsApp huwa yanawasilisha umoja wa watu kuwa na malengo yanayofanana.

Mfano makundi ya shule na vyuo huwa hayana dhamira ya kutaka kusalimiana na kujuliana hali, bali yapo pale maalum kupima mafanikio ya walio kwenye kundi.




Wanawake wajasiriamali kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Iramba mkoani Singida wakiwa na vyerehani ambavyo walipewa juzi na Shirika lisilo la kiserikali la Brac Maendeleo Tanzania (BMT) kupitia mradi wake wa kuwawezesha wanawake na mabinti balehe kiuchumi (AIM). **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

## Wanawake, wasichana wawezeshwa kiuchumi

**Na Mwandishi Wetu,** SINGIDA

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Brac Maendeleo Tanzania (BMT) limetumia Sh. 294,823,389 kuwawezesha wanawake na wasichana balehe kiuchumi wa Mkoa wa Singida kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024.

Meneja wa shirika hilo wa mkoa huo, Isihaka Mirambo, aliyasema hayo wakati wa kukabidhi vifaa mbalimbali vikiwamo vyerahani kwa wanufaika. Mirambo, alisema shirika hilo lilitoa kiasi hicho cha fedha kupitia mradi wake wa Kuwawezesha Wanawake na Mabinti Barehe Kiuchumi (AIM) na kujikwamua na hali ngumu ya maisha kutokana na kukosa kipato.

Alisema AIM ambao sasa umehitimishwa kwa Mkoa wa Singida ulikuwa ukitekelezwa katika Halmashauri za Wilaya ya Iramba, Manyoni na Manispaa ya Singida kuanzia Julai mwaka juzi.

Alisema katika kipindi hicho shughuli zilizofanyika katika halmashauri hizo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo serikali ya Mkoa wa Singida na halmashauri ni uwezeshwaji kijamii, kiuchumi na Uchechemuzi.

Mirambo, alisema katika kipengele cha uwezeshaji kijamii, mradi huo ulilenga kutoa elimu juu ya masuala mtambuka ya kijamii ili kuwajengea uwezo wa kujiamini, kuchanganua na kutatua changamoto zinazowazunguka wasichana na wanawake.

"Washiri katika kipengele hiki waliweza kupewa elimu juu ya masuala ya afya ya uzazi, athari zitokanazo na matumizi ya dawa za kulevya, mimba za utotoni , ujasiriamali na elimu ya fedha ambapo jumla ya wshiriki 3,787 walinufaika," alisema Mirambo.

Alisema katika uwezeshaji huo wa kijami, vijana 72 wa kike na wa kiume walipata ajira ya muda kwa ajili ya kusaidia uwezeshaji.

Mirambo aliongeza kuwa katika uwezeshaji kiuchumi. watu 1,429 wamenufaika, shughuli hiyo ililenga kuwawezesha wanawake na wasichana kiuchumi kwa kuwapatia elimu na mafunzo, nyenzo ambazo wamechagua wenyewe katika sekta ya kilimo, ufugaji na biashara ndogo ndogo.

Alisema shirika hilo lilianzisha vikundi vya vikoba kama sehemu ya kuwawezesha wanawake na wasichana kiuchumi na kuwa na uwezo wa kujikimu katika hali ya dharura.

Mirambo, alisema mpaka sasa vikundi 60 vilivyoanzishwa na kusajiliwa katika halmashauri husika na vina wanachama 983, akiba mpaka kufikia Novemba mwaka jana Sh.Milioni 91.5, mikopo iliyotolewa Sh. milioni 7.155 na wakopaji ni 239.

BRAC Maendeleo limetoa mitungi ya gesi 179 ili kuunga mkono serikali kampeni yake ya matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa kuwawezesha wasichana na wanawake kujihusisha na biashara ndogondogo na kujipatia kipato.

# Askofu: Wanaoua watoto wakamatwe

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

ASKOFU Mkuu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Dodoma, Beatus Kinyaiya amewataka wazazi na walezi kuisaidia serikali kutoa taarifa sahihi dhidi ya ukatili wa watoto wadogo na kuuawa ili watuhumiwa wakamatwe na kuchukuliwa hatua.

Aidha, Askofu Kinyaiya amesema wazazi na walezi wanapaswa kuwa mstari wa mbele kujenga msingi mzuri wa maadili ya vijana tangu awali ili kuwaandaa kuwa viongozi bora wa baadaye.

Alitoa rai hiyo katika Sikukuu ya Familia Takatifu iliyokwenda sambamba na ufunguzi wa Jubilei Kuu ya mwaka 2025 ya Ukristo Kijimbo iliyofanyika katika Kanisa la Mtakatifu Paulo wa Msalaba jimboni humo.

Alisema kwa sasa kumekuwa na matukio mengi ya ukatili wa kijinsia ikiwemo mauaji ya watoto, kuchomwa moto, vitendo ambavyo kamwe havikubaliki kwenye jamii,hivyo wazazi wanapaswa kushirikiana na serikali kuwafichua wahalifu hao.

"Hivi vitendo vya kikatili havikubaliki kabisa katika jamii, naomba wazazi na walezi tuunge mkono jitihada za serikali za kupambana na ukatili wa kijinsia kwa kutoa taarifa pale mnapoona kuna uhalifu wa aina hiyo unatendeka," alisema Askofu Kinyaiya.

Alisema kila mmoja ana kila sababu ya kuwalinda watoto wadogo, hivyo wanapobaini wako katika mazingira hatarishi wanapaswa kutoa taarifa mapema kabla hawajadhurika.

Akizungumzia kuhusu vijana, aliwataka wazazi wasikate tamaa kuwapa maadili na malezi mazuri kwa sababu yatawasaidia kwa siku za baadaye.

Alisema wazazi na walezi hawapaswi kukata tamaa katika malezi ya vijana na wasiwaache wakishinda mitandaoni kuiga mambo yasiyofaa kwani ni kinyume na maadili ya Kitanzania.

Aliwakumbusha wazazi na walezi kutenga muda wa kukaa na familia zao kuwapa vijana busara, kuwafundisha kufanya matendo ya huruma ambayo yatawajenga katika misingi ya maadili bora.

Aliwakumbusha pia vijana kujenga utaratibu wa kukaa na wazazi wao ili kuchota busara ambazo zitawasaidia kuendesha maisha yao na familia zao kwa baadaye.

Kwa upande mwingine nyingine; Askofu Kinyaiya, aliwakumbusha waumini wa kanisa hilo kufanya matendo ya huruma kwa kuwapatia watoto yatima misaada ili nao wajisikie amani kama ilivyo kwa watoto wengine.

Alisema waumini na jamii wakifanya hivyo, watasaidia kuwajenga watoto na vijana katika misingi ya kutambua nini maana ya upendo unaopaswa kutendeka katika jamii.





# Marufuku wagonjwa kutozwa fedha za mafuta, posho

**Na Elizabeth John,**
WANGING'OMBE

SERIKALI imepiga marufuku halmashauri na vituo vya afya nchini kutoza fedha za mafuta na posho kwa wagonjwa kwa ajili ya kupata huduma ya gari ya kubeba wagonjwa wakati wa rufani.

Amri hiyo ilitolewa juzi na Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Wanging'ombe wakati akikabidhi gari la wagonjwa kwa Kituo cha Afya Makoga.

Dk. Dungange, aliiomba Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe kuhakikisha gari hilo linakuwa zima na mafuta siku zote ili wananchi waweze kupata huduma bila vikwazo.

"Ni marufuku kwa mgonjwa kutozwa fedha yeyote kwa ajili ya kutumia gari hili, hili ni gari la serikali kwa ajili ya rufani ya wagonjwa na limeletwa kwa ajili hiyo sio kutoza hata shilingi moja," alisema Dk. Dungange.

Alisema mwananchi atakayetozwa fedha, atoe taarifa ili serikali ichukue hatua.

Awali Mganga Mfawidhi wa kituo hicho, Dk. Joseph Sota, alisema licha ya kazi kubwa wanayoifanya kuwahudumia wananchi, wanakabiliwa na adha ya kukosa umeme mbadala hali inayopelekea kushindwa kutoa baadhi ya huduma ikiwamo upasuaji umeme ukikatika usiku.

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Dk. Peter Nyanja, aliahidi kutatua baadhi ya changamoto zilizo ndani ya uwezo wao kwa fedha za mapato ya ndani.

Baadhi ya wakazi, akiwamo Debora Mgina, aliishukuru serikali kwa kuwapelekea gari hilo na kuondokana na kero ya kukosa usafiri.

"Tunaishukuru serikali kwa sababu huko nyuma tulikuwa tunalazimika kukodi magari ya watu kwa gharama kubwa," alisema Debora.



Baadhi ya wakazi wa Kata ya Ifumbo katika Halmashauri ya Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, wakiendelea kuchimba madini ya dhahabu kwenye mkondo wa Mto Zira juzi, hali inayosababisha uharibifu wa mazingira kwenye mto huo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Watakaoharibu uandikishaji wapigakura waonywa

**Na Mwandishi Wetu,**
NJOMBE

TUME Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC) imewaonya wananchi kuacha tabia ya kujiandikisha kuwa mpiga kura zaidi ya mara moja kwa kuwa ni kosa la jinai kwa mujibu wa sheria.

Onyo hilo lilitolewa jana na Mkurugenzi wa Kitengo cha Huduma ya Taifa ya Uchaguzi wa INEC, Mtibora Selemani kwa niaba ya Mwenyekiti wa Tume Huru ya Taifa Uchaguzi, Jaji Jacobs Mwambegele kwenye mkutano wa tume na wadau wa uchaguzi kuhusu uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura katika uchaguzi mkuu mwakani.

Selemani, alisema kujiandikisha zaidi ya mara moja katika daftari hilo kosa la jinai kifungu 114 (1) cha sheria ya uchaguzi huo wa rais, wabunge na madiwani Namba 1 ya mwaka 2024.

Alisema kifungu hicho kinaeleza kuwa, mtu yeyote atakayejiandikisha zaidi ya mara moja, atakuwa ametenda kosa la jinai na akitiwa hatiani, adhabu yake ni faini isiyopungua Shilingi 100,000 na isiyozidi Shilingi 300,000 au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita na kisichozidi miaka miwili gerezani au vyote kwa pamoja.

Selemani, aliwataka wadau wa mkutano huo kwenda kutoa elimu kwa wananchi wajiandikishe mara moja na kwenye kituo kimoja ili kuepuka uvunjaji wa sheria.

"Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 168 cha sheria ya uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Namba 1 ya mwaka 2024 kadi ya mpigakura zilizotolewa mwaka 2015 na 2020 zenye jina la Tume ya Taifa ya Uchaguzi ni halali na zitaendelea kutumika kwenye chaguzi zijazo, hivyo zoezi hili la uboreshaji haliwahusu wapigakura wenye kadi hizo," alisema Selemani.

Alisema tume imeweka utaratibu kwa watu wenye ulemavu, wazee, wagonjwa, wajawazito na wakina mama wenye watoto wachanga wanaokwenda nao vituoni kupewa fursa ya kuhudumia bila ya kupanga foleni.

"Tunawaomba wadau wa uchaguzi muwafahamishe wananchi wote waliopo kwenye makundi tajwa kujitokeza kwa wingi kwenda kujiandikisha au koboresha taarifa zao vituoni kwa kuwa utaratibu mzuri wa kuwahudumia umewekwa," alisema Selemani.

Alisema tume hiyo katika kuhakikisha inakwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia ikiwa ni pamoja na kurahisisha zoezi hilo, imeboresha mfumo wa uandikishaji ambao kwa mara ya kwanza utamwezesha mpigakura aliyepo kwenye daftari kuainisha mchakato wa kuboresha taarifa zake au kuhama kituo kwa kutumia aina yeyote ya simu ya kiganjani au kompyuta.

Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Usimamizi wa Uchaguzi wa tume hiyo, Stephen Elisante, alisema katika mkoa huo watu 80,994 wanatarajiwa kujiandikisha katika daftari hilo na kuwataka vijana kuhamasishana na kujiepusha na upotoshaji.

Kauli mbiu ya uboreshaji wa daftari hilo kwa mwaka 2024/25: "KUJIANDIKISHA KUWA MPIGAKURA NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA".

## Washauriwa kuwekeza taasisi za fedha

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAKAZI mkoani hapa wameshauriwa kujenga utamaduni wa kuwekeza fedha zao kwenye taasisi za fedha ili kupata gawio.

Ushauri huo ulitolewa juzi na Mkuu wa Wilaya ya Wanging'ombe, Zakaria Mwansasu kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka katika uzinduzi wa Mfuko wa Hati Fungani Samia unaolenga kuboresha barabara zilizo chini ya Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) kwa kushirikiana na Benki ya CRDB.

Mwanasasu, alisema kuweka fedha kwenye taasisi za fedha kunasaidia kuwa salama na kupata faida na sio kufukia ndani ya nyumba kwa kuwa sio sehemu salama.

"Nawaomba tuachane na ule utamaduni wa kufukia fedha, tuachane na ule utamaduni wa kulala na fedha kwenye viroba na mahali salama ambapo utaziweka fedha ni kwenye hati fungani kwa sababu ukiweka pale una uhakika hii fedha itanilipa," alisema Mwansasu.

Alisema kuzinduliwa kwa mfuko huo ni dhahiri utatuzi wa changamoto ya miundombinu hususan mkoani Njombe unakwenda kutatuliwa kwa wakati na wakandarasi.

"Ujenzi wa barabara zetu utakamilika kwa wakati na kuhakikisha fedha za kazi na kuwalipa wakandarasi wa ndani zinapatikana bila ya kuchelewa," alisema.

Meneja wa CRDB Kanda za Nyanda za Juu, Jeniffer Tondi, alisema hati fungani hiyo ya miaka mitano italeta manufaa makubwa zaidi katika uwekezaji wa fedha.

"Watanzania walioko nje pia tunawahimiza walete fedha nyumbani na wawekeze hapa sehemu ambayo ni salama na wao pia watakuwa ni sehemu ya kuchochea maendeleo katika nchi yao," alisema Jeniffer.

Mmoja wa washiriki wa uzinduzi huo, Ester Fredrick, alisema hati fungani ni muhimu na sio kwa taifa pekee hata kwa mtu binafsi kwa sababu anaweza kupata faida kubwa zaidi kuliko kubaki na hela ndani ambazo hazizalishi chochote.

Katika uzinduzi huo ulioudhuriwa na viongozi wa taasisi mbalimbali za umma na wafanyabiashara binafsi Njombe umechangia Shilingi bilioni 2.3.





## KMKM yatakiwa kudhibiti magendo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KIKOSI cha Kuzuia Magendo Zanzibar (KMKM) kimetakiwa kudhibiti magendo na uhalifu katika ukanda wa bahari na nchi kavu visiwani hapa.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Ikulu, Ali Suleiman Mrembo wakati akifungua jengo la utawala la kambi ya KMKM lililopo Bwefum Wilaya ya Magharibi 'B' Unguja.

Mrembo, alisema kuwapo kambi hiyo katika ukanda huo kutaondoa malalamiko ya kukithiri vitendo vya uhalifu katika maeneo ya bandari bubu za Kisakasaka, Nyamanzi, Fuoni Kibondeni, Bungi na Kikungwi yakitumika kama ni mlango wa kuingia wahalifu.

Alisema maeneo hayo pia yanatumika kusafirisha bidhaa za wizi, kuingiza dawa ya kulevya hususani bangi na mirungi na kuingiza bidhaa za magendo.

Mrembo, alisema kwa kuwa maofisa hao wanaongozwa na nidhamu, uadilifu, uwajibikaji na kujitolea, anaamini hakutakuwa na manung'uniko kwa wananchi dhidi ya serikali kuruhusu aina yoyote ya magendo.

"Wapo baadhi ya watu wanatumia njia ya bandari ukanda huu wa Fumba kuingiza madawa ya kulevya, uvuvi haramu, utumiaji wa bandari bubu kwa lengo la kukwepa kodi ya serikali," alisema.

Aliwataka wananchi kushirikiana na KMKM kupeana kuhakikisha ustawi wa usalama wa wananchi wanaotumia bahari unaimarika.

Akizungumzia Miaka 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar, alisema ufunguzi wa jengo hilo ni utekelezaji wa vitendo wa malengo halisi ambayo muasisi wake, Abeid Aman Karume kuona wananchi wanyonge wanaishi mazingira mazuri na salama na kushiriki katika kazi za uzalishaji na ujenzi wa taifa lao.

Mkuu KMKM, Azana Hassan Msingiri, alisema majengo hayo ni malengo ya serikali kuboresha mazingira ya ufanyakaji kazi kwa kubadilisha taswira na mazingira ya kambi kwa wapiganaji wake.

Akizungumzia ujenzi wa kambi hiyo, Katibu Mkuu, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Issa Mahfoudh Haji, alisema ni muendelezo na ukarabati wa majengo ya KMKM Unguja na Pemba ili kuimarisha mazingira ya kazi kwa idara maalum za Serikali ya Mapinduzi Zanizbar (SMZ).

Kwa mujibu wa Haji, mradi huo ulianza Febuari 4, mwaka jana na kukamilika mwanzoni mwa Disemba mwaka jana kwa gharamu ya zaidi ya Sh. bilioni 1.16.

# Ufaulu darasa la saba waongezeka Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BARAZA la Mitihani Zanzibar limetangaza matokeo ya mtihani wa darasa la saba mwaka jana yakionyesha ufaulu umepanda kwa asilimia 1.66 kutoka asilimia 95 ya mwaka juzi.

Akitangaza matokeo hayo kwa waandishi wa habari katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Mazizini visiwani hapa, Mkurugenzi Mtendaji Baraza hilo, Dk. Rashid Abdulazizi Mukki, alisema watahiniwa 44,486 sawa na asilimia 96.66 wamefaulu mtihani huo kwa madaraja ya A,B,C na D kati ya watahiniwa 46,021 waliofanya mtihani wa darasa la saba mwaka jana.

Mukki, alisema kati ya watahiniwa waliofaulu, wanaume ni 20, 571 sawa na asilimia 46 24 na wanawake 23,915 sawa na asilimia 53.76.

Alisema watahaniwa 1,535 sawa na asilimia 3.34 wamepata daraja la F, idadi hiyo imepungua kwa asilimia 1.66 kutoka 5.00 mwaka 2023 hadi 3.34 mwaka 2024.

Akitaja ubora wa ufaulu kwa wastani, alisema watahaniwa 228 wamefaulu kwa wastani wa daraja A, 4,816, daraja B, 20,459, daraja C, 18,983, daraja la D na watahiniwa 1,535 wastani wa chini wa daraja la F.

Akizungumzia ufaulu wa masomo kwa ujumla kwa mwaka jana, alisema somo la Creative Arts and Sports na Social Sience ni yenye ufaulu wa juu zaidi ya asilimia 99.68 ikilinganishwa na mwaka juzi yalikuwa na na ufaulu wa asilimia 99.86.

Alisema somo la Lugha ya Kiswahili ufaulu umepanda kutoka asilimia 89.32 mwaka juzi hadi asilimia 94.89 mwaka jana.

Alisema somo la hisabati ufaulu umepanda kutoka asilimia 50.10 mwaka juzi hadi asilimia 55.52 mwaka huu.

Kuhusu tuhuma za udanganyifu, alisema kumebainika viashiria kwa watahiniwa 642 katika vituo 25.

Alisema matokeo ya watahiniwa hayo yamezuiliwa kwa mujibu wa kifungu cha 57(b) cha kanuni za baraza hilo ya mwaka 2014.

Alisema uchunguzi ukikamilika, watahiniwa watakaopatikana na hatia watafutiwa na wasimamizi wa mitihani kuchukuliwa hatua.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, akipata ufafanuzi kuhusu ujenzi wa Kituo cha Afya Kiuyu Minungwini, Mkoa wa Kaskazini Pemba ikiwa ni shamrashamra za Miaka 61 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya mwaka 1964 baada ya kuweka jiwe la msingi jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mkandarasi abanwa ujenzi kituo cha afya

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, ameemtaka mkandarasi kukamilisha haraka ujenzi wa Kituo cha Afya Kiuyu Minungwini ili wananchi waendelee kufaidika na matunda ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Abdullah alitoa kauli hiyo jana wakati akiweka jiwe la msingi la ujenzi wa kituo hicho kilichoko Wilaya ya Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba ikiwa ni shamra shamra za kutimiza Miaka 61 ya Mapinduzi hayo.

Alisema mkandarasi huyo anatakiwa kuhakikisha anakamilisha ujenzi huo na kukabidhi kituo hicho kwa wakati ili wakazi wa Kiuyu Minungwini na maeneo jirani wapate huduma ya afya .

Abdullah, alisema serikali inawekeza fedha nyingi katika sekta ya afya kwa kujenga na kuboresha miundombinu ya afya na kununua vifaa vya kisasa kwa lengo la kutoa huduma bora kwa wananchi ikiwa ni azma ya Mapinduzi ya mwaka 1964.

Aliwataka wananchi kushirikiana kuyalinda na kuyatetea Mapinduzi hayo yaliyowakomboa kutoka katika makucha ya wakoloni.

Vilevile, aliwataka wakazi hao na maeneo mengine kuwa walinzi wa miundombinu inayoendelea kujengwa katika maeneo yao na kuacha jazba zinazopelekea uharibifu na gharama kwa serikali.

Naibu Waziri wa Wizara ya Afya, Hassan Khamis Hafidh, alisema serikali imejenga hospitali za wilaya na mkoa kisiwani Pemba kwa ubora na viwango vya kitabibu.

Hafidh, alisema pia imeweka madaktari bingwa, huduma ya wagonjwa wanaohitaji uangali maalum (ICU), huduma za mionzi, upasuaji, usafishaji ili kuimarisha huduma za matibabu kisiwani humo.

Alisema wizara hiyo itaendelea kubuni miradi ya maendeleo katika sekta ya afya ili wananchi wa Unguja na Pemba wapate huduma bora za afya na kwa wakati.

Akitoa taarifa ya ujenzi wa kituo hicho, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Mngereza Mzee Miraji, alisema ukikamilika, utawanufaisha wananchi wa Minungwini na maeneo ya Mkoa wa Kaskazini Pemba kwa kupata huduma za

Miraji, alisema kituo hicho cha ghorofa moja, kinajengwa kwa ushirikiano wa Serikali ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa zaidi ya shilingi Bilioni 1.7.



Bingwa wa Magonjwa ya Macho kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili, (MNH), Dk. Rogers Sempinduna, akimfanyia upasuaji wa mtoto wa jicho mmoja wa wagonjwa katika Hosptali ya St Joseph Peramiho, mkoani Ruvuma katika kambi ya siku nne, iliyoandaliwa na MNH pamoja na halmashauri ya Wilaya ya Songea. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## MAUAJI KADA CCM:

# Mahakama Kuu yawaachia huru wanachama watatu wa CHADEMA

**Na Elizabeth John, NJOMBE**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Iringa imewaachia huru wanachama watatu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) waliokuwa wanakabiliwa na kesi ya mauaji ya kada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Emmanuel Mlelwa.

Hao ni Geogre Sanga, Goodluck Mfuse na Optatus Nkwera walioshtakiwa kwa mauaji ya Emmanuel Mlelwa yaliyofanywa Septemba 2020.

Katika kesi hiyo ya jinai namba 5236/2024, upande wa Jamhuri uliwakilishwa na Wakili Mkuu wa Serikali Cesilia Mkonongo, akisaidiwa na Geres Tesha na Elise James huku upande wa utetezi ukiwakilishwa na Wakili Dickson Matata, akisaidiwa na Franki Ngafumika, Innocent Kibadu na Neema Msafiri.

Akisoma hukumu hiyo jana kwa njia ya mtandao, Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Iringa inayojumuisha pia mkoa wa Njombe, Danstan Ndunguru, alisema kuachiwa huru kwa watuhumiwa hao kunatokana na upande wa Jamhuri kushindwa kuthibitisha kosa dhidi ya Gegore Sanga na wenzake.

Alisema upande wa utetezi ulikuwa na mashahidi watano huku upande wa Jamhuri ukiwa na mashahidi 14 na kwamba hakuna shahidi aliyeona watuhumiwa wakitenda kosa la mauaji ya Emmanuel Mlelwa.

Jaji huyo alisema kuwa katika ushahidi wa kimazingira uliowasilishwa mahakamani na upande wa Jamhuri, haukuwa na muunganiko mzuri usioacha shaka.

Alisema ushahidi huo wa kimazingira umeacha shaka iliyofanya mahakama ishindwe kubaini iwapo ushahidi wa kimazingira uliotolewa, kuwaunganisha watuhumiwa na kosa ni sahihi au la.

Jaji Ndunguru alisema ushahidi wa kisayansi wa uchunguzi wa vinasaba ulioletwa mahakamani umeshindwa kutumika kuwatia hatiani washtakiwa hao kwa kuwa sampuli za vinasaba zilizopelekwa kwa Mkemia Mkuu wa Serikali, wakati zinachukuliwa kulikuwa na ukiukwaji taratibu za kisheria kwa mujibu wa Sheria ya Vinasaba ya Mwaka 2009.

Baada ya hukumu hiyo, Mwenyekiti wa Kanda ya Nyasa ya CHADEMA, Joseph Mbilinyi, maarufu Sugu, alitaka serikali kumaliza kesi alizoziita "za wafungwa wa kisiasa" katika maeneo mengine nchini, ikiwamo ya Kibaha mkoani Pwani, akidai zinachafua taswira ya nchi.

# BMH yaokoa bil. 1.6/- upandikizaji figo

**Na Renatha Msungu DODOMA**

HOSPITALI ya Rufani ya Kanda ya Benjamini Mkapa (BMH), imeokoa Sh. bilioni 1.6 baada ya kufanya upandikizaji wa figo kwa wagonjwa 50 waliokuwa na matatizo hayo kutoka maeneo mbalimbali nchini.

Mkurugenzi Mtendaji wa BMH, Prof. Abel Makubi, wakati akitoa taarifa ya upandikizaji wa figo kwa mafanikio kwa mgonjwa Emmanuel Woiso aliyefanyiwa upandikizaji na madaktari bingwa kutoka BMH.

Prof. Makubi alisema BMH itaendelea kupandikiza figo kwa wagonjwa mbalimbali wanaofika hospitalini hapo kupitia wataalamu wabobezi, lengo kuu likiwa ni kuhakikisha wanaokoa maisha ya wagonjwa wenye tatizo la figo.

Pia alisema hospitali hiyo itaendelea kuvuna figo kwa njia ya matundu ili kuhakikisha wagonjwa wanaoletwa hospitalini hapo wananufaika na matibabu ya upandikizaji kutoka kwa madaktari bingwa.

"Tunashukuru uwekezaji unaofanywa na serikali kwenye sekta ya afya ambao unapelekea matibabu haya yanafanyika kwa wagonjwa wanaohudhuria hospitalini hapo,"alisema Prof. Makubi.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Figo, Sabina Mmbali, alisema wamefanikiwa kumruhusu mgonjwa wa 50 ambaye alipandikizwa figo hospitalini hapo, kitendo ambacho kinawapa faraja kutokana na kazi yao kuleta matokeo chanya.

"Jana tumemruhusu Emmanuel ambaye amepandikizwa figo na hali yake inaendea vizuri. Hii inatufanya tuzidi kuwajibika katika majukumu yetu kwa sababu tunaowafanyia upandikizaji wanaendelea vizuri na maisha," alisema Dk. Mmbali.

Alisema BMH itaendelea kutoa matibabu hayo kwa wagonjwa wanaojitokeza kupata matibabu ili kuhakikisha wanarejea katika majukumu yao ya kila siku ya kujiinua kiuchumi pamoja na familia zao.

Hata hivyo, aliitaka jamii kuhakikisha kuwaleta wagonjwa BMH wenye dalili za magonjwa ya figo ili kufanyiwa uchunguzi na kupatiwa matibabu.

Emmanuel Woiso ambaye ni mnufaika wa upandikizwaji figo katika BMH, aliwashukuru madaktari bingwa wa figo pamoja na wataalam wa afya kutoka hospitalini hapo.

Woiso alisema baada ya kupandikizwa figo hivi sasa hali yake inaendelea vizuri, huku akiwashukuru madaktari wa hospitali hiyo kutokana na huduma nzuri alizopatiwa.

Aidha, aliwataka jamii kutosita kwenda hospitalini hapo kufanyiwa vipimo ili kubaini kama wanatatizo la figo ili waweze kupatiwa matibabu na wataalamu kutoka BMH.


## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**AMINA RAMADHANI KINANA,**
Anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya Hajoe yenye namba za usajili MC 976 DVC, CHASSIS NAMBA LC6PCJK28N0A79336, ENGINE NAMBA 156FMI5AD3F64104. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi.
**TAARIFA YA POLISI: PHQ/DOD/DOD/58609/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**FILEX PERFECT CHAMI**
anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili MC 637 DTX aina ya Kinglion, Chassis namba LZLISP909NHA00548, Engine namba KL162FMJ 220600548 Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**TAARIFA YA POLISI: PHQ/MAN/BAB/12168/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GAI ABED GAMBA**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE USAJILI T 987 DCY AINA YA TOYOTA CARINA YENYE RANGI YA FEDHA KWA YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA KADI HIYO ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI TAARIFA
**PHQ/IRI/MUF/20764/2024.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA ILALA**
**(JENGO LA WIZARA YA ARDHI – KIVUKONI)**
**MAOMBI MADOGO NAMBA. 256/2024**
**JULIUS CHIPALA NYAMAKWELO..................MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**SHARIFA OTHMAN KHALID.................MJIBU MOMBI NA. 1**
**TUJIJENGE TANZANIA LTD.................MJIBU MAOMBI NA. 2**
**JUCACO AUCTION MARTH DEBT COLLECTOR & COURT BROKERS LIMITED..................MJIBU MAOMBI NA. 3**

**KUITWA SHAURINI**

**TUJIJENGE TANZANIA LIMITED**
**JUCACO AUCTION MARTH DEBT COLLECTOR & COURT BROKERS LIMITED..................POPOTE MLIPO**

JULIUS CHIPALA NYAMAKWELO amewasilisha shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Ilala lililopo (Jengo la Wizara ya Ardhi – Kivukoni). Maombi hayo yamepangwa kutajwa tarehe 22/01/2025 saa 8:00 mchana. Hivyo basi unatakiwa wewe mwenyewe au wakili wako kuleta kiapo kinzani "counter affidavit" ndani ya siku 7 kuanzia tarehe ya tangazo hili kutolewa. Vielelezo vyote vinavyohusu shauri tajwa vinapatikana katika Masijala ya wazi ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Ilala. Endapo hautatekeleza haya, maombi hayo yatasikilizwa upande mmoja na uamuzi/amri kutolewa.

Imetolewa na kutiwa muhuri wa Baraza leo tarehe 31 Mwezi Disemba, Mwaka 2024.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) – ILALA
DAR ES SALAAM

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PATSON EDSON MBEWE**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE USAJILI T993 AQP HIVYO ANATOA WITO KWA YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA KADI HIYO ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI TAARIFA
**PHQ/IRI/IRI/20755/2024.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**MAHAKAMA YA WILAYA DODOMA**
**RUFAA/MADAI NAMBA 3/2023**
**Shauri ya Rufaa Madai Namba 3/2023**
**Katika Mahakama ya wilaya ya DODOMA**
**RICHARD NSALAMBI..........................MRUFANI**
**DHIDI YA**
**ZUENA MSEKWA...............................MRUFANIWA**

**Kwa: ZUENA MSEKWA**

Kwa rufaa iliyotajwa hapo juu itasikilizwa katika Mahakama iliyotajwa hapo juu siku ya JUMATANO tarehe 8 Mwezi 1 Mwaka 2025 unatakiwa uhudhurie katika Mahakama hiyo Mrufani/Mrufaniwa/ Shahidi pamoja na vielelezo vyovyote kama vipo.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Muhuri wa Mahakama hii leo.
Tarehe 20... Mwezi 12......Mwaka 2024

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA WILAYA
DODOMA

HABARIKIMATAIFA

# Makombora yarindima Ukraine

**KYIV, Ukraine**

RUSSIA imefanya mashambulizi mapya makubwa ya anga dhidi ya maeneo mbalimbali ya Ukraine kwa kutumia makombora mazito.

Mifumo ya ufuatiliaji habari za kivita za Ukreni ziliripoti kuwa mashambulizi hayo yalihusisha makombora ya cruise na balestiki na milipuko mipya iliyozinduliwa hivi karibuni.

Milipuko ilisikika katika mkoa wa Kyiv, Sumy na maeneo mengine.

Aidha kuna ripoti za kurushwa kwa makombora ya aeroballistic ya Kinzhal kutoka kwenye ndege ya MiG-31.

Jeshi la Ukraine pia linaripoti kuwa ndege sita za Russia za mashambulizi ya kimkakati zilizosafiri kwenye anga lake zilirusha makombora.

Watu saba walijeruhiwa katika eneo la Kherson kutokana na mashambulizi ya makombora hayo, huku majengo kadhaa yakiharibiwa.

Jeshi la Ukraine lilisema kwamba wakati wa kujibu mashambulizi hayo, vifusi vya roketi viliangukia kwenye nyumba za watu binafsi kusini mashariki mwa mji mkuu.

Wakati huo huo, Russia na Ukraine zimebadilishana wafungwa wa kivita katika makubaliano yaliyofikiwa juzi.

Mamia ya wafungwa wameachiliwa huru kupitia mpango uliosimamiwa na Umoja wa Falme za Kiarabu.

Rais wa Ukraine Volodymir Zelensky, alisema wafungwa 189 wa Ukraine, wakiwemo maofisa wa kijeshi, wanajeshi wanaolinda mpaka na raia wawili, waliachiwa. Kiongozi huyo aliushukuru Umoja wa Falme za Kiarabu kwa kufanikisha mabadilishano hayo. Wizara ya Ulinzi ya Russia, kwa upande wake ilisema wanajeshi wao 150 waliachiliwa huru kama sehemu ya ubadilishanaji huo ambao kila upande uliwaachia watu 150.

Nchi hizo mbili zimefanya mabadilishano ya wanawajeshi mara kadhaa wakati wa vita hivyo vinavyoendelea kwa karibu miaka mitatu.

Kilichosababisha kutofautiana kwa idadi hiyo bado hakijawa wazi. Russia ilisema askari wake kwanza walipelekwa kwenye mpaka wa Belarus, ambako walipewa msaada wa kisaikolojia na matibabu kabla ya kupelekwa Urusi.

***BBC***



Baba wa mtoto aliyefariki kutokana na baridi kali Ukanda wa Gaza akibeba mwili kwenda kuzika jirani na kambi yao. **PICHA: REUTERS**

# Idadi ya watoto waliofariki kwa baridi Gaza yaongezeka

**GAZA, Palestina**

IDADI ya watoto wanaofariki kwa baridi kali katika Ukanda wa Gaza imefikia tisa na kuongeza hofu kwa Wapalestina wanaoteseka na hali hiyo ya kutisha.

Taarifa zilizotolewa jana na Wizara ya Afya ya Gaza, ilisema mototo mwenye umri wa chini ya wiki tatu alifariki jana akiwa mikononi mwa mama yake.

„Niliamka asubuhi na kumwambia mume wangu kuwa mtoto alikuwa hajatikisika kwa muda. Alifunua uso wake na kumkuta amekuwa wa bluu, ametafuna ulimi, huku damu zikimtoka mdomoni," alisema Nariman al-Najmeh.

Akizungumza akiwa katika hema lao lililowekwa ufukweni mwa bahari kusini mwa Gaza, Nariman alisema ndani ya hema wanaishi na mumewe na watoto wao wawili wadogo.

Kifo hicho kinafikisha idadi ya watoto waliofariki kutokana na baridi kali Gaza ndani ya kipindi cha wiki mbili

Wakati huo huo, Mkuu wa Shirika la afya Ulimwenguni (WHO) Edros Ghebreyesus, alitoa wito wa kukomeshwa kwa mashambulizi katika hospitali katika Ukanda wa Gaza.

Ghebreyesus alisema kuwa hospitali za Gaza kwa mara nyingine tena zimekuwa uwanja wa vita na kwamba mfumo wa afya umerudi chini na kuwa tishio.

Madai ya Ghebreyesus yanakuja baada ya jeshi la Israel kushambulia na kuhamishwa kwa Hospitali ya Kamal Adwan Ijumaa iliyopita.

Hospitali hiyo imekuwa kituo kikubwa cha mwisho cha afya kinachofanya kazi kaskazini mwa Ukanda wa Gaza, licha ya mashambulizi kukumba hospitali mbili katika mji wa Gaza siku ya Jumapili.

Jeshi la Israel lilisema kuwa maeneo hayo mawili yanatumiwa na Hamas kama vituo vya kutoa amri ya mapigano, jambo ambalo vuguvugu hilo limekanusha mara kwa mara.

Mkurugenzi huyo wa Shirika la Afya Ulimwenguni alitoa wito huo baada ya mashirika ya kutetea haki za binadamu kulalamika wakitaka kuachiliwa kwa mkurugenzi wa Hospitali ya Kamal Adwan, Dk Hossam Abu Safiya, ambaye alikamatwa na vikosi vya Israeli wakati wa mashambulizi dhidi ya hospitali hiyo.

***BBC***

## Jimmy Carter pembeni ya mke wake

**WASHINGTON, Marekani**

MAZISHI ya kitaifa ya rais wa zamani wa Marekani, Jimmy Carter, aliyefariki Jumapili akiwa na umri wa miaka 100, yatafanyika januari 9, katika Kanisa Kuu la Katoliki jijini Washington.

Rais wa Marekani Joe Biden, ambaye mwaka jana alisema Carter alimuomba atoe hotuba ya hadithi ya maisha kwenye mazishi yake, aliagiza kwamba Januari 9 iwe ya maombolezo ya kitaifa.

Hata hivyo serikali ilianza siku sita za shughuli za mazishi rasmi ya kitaifa ya kiongozi huyo.

Jeshi la Marekani, lilisema mwili wa kiongozi huyo utasafirishwa kwa msafara wa magari kupitia mji aliozaliwa wa Plains, katika jimbo la Georgia na utasimama katika shamba alikokulia.

Kisha mwili wa Carter utasafirishwa hadi Atlanta, ambako utalala katika Kituo cha Carter hadi asubuhi ya Januari 7.

Baadaye mwili utasafirishwa hadi Washington, DC ambako utalazwa katika majengo ya Bunge la Marekani ya Capitol Hill hadi pale itakapofanyika ibada ya kuuaga.

Kiongozi huyo atazikwa katika makaburi ya Georgia Januari 9, mbembeni alipozikwa mke wake Rosalynn Carter.

***DW***

## Polisi yavunja maandamano kupinga utekaji watu Kenya

**NAIROBI, Kenya**

JESHI la Polisi Kenya, limesambaratisha kwa mabomu ya machozi waandamanaji waliongia mitaani kupinga kuongezeka kwa wimbi la utekaji nyara

Shirika la habari la Uingereza la Reuters, lilisema waandamani hao walikusanyika katika viunga vya mji mkuu wa Naribu kupinga kupotea kwa wakosoaji wa serikali ya William Ruto.

Kwa mujibu wa mashirika ya kutetea haki za binadamu, watu kadhaa wametekwa nyara katika miezi ya hivi karibuni, wengi wao wakiwa wanakosoa polisi na idara za ujasusi kwa kuhusika na matukio hayo.

Mamlaka za Kenya zimejitokeza na kujibu shutuma hizo zikidai kuwa serikali haiungi mkono na wala haihusiki kwa namna yeyote kuhusu mauaji ya kiholela pamoja na utekaji nyara.

***DW***

# Yanga Princess yanyakua wachezaji Simba

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga Princess imekamilisha usajili wa wachezaji wawili wa timu ambao msimu uliopita walikuwa wakiichezea Simba Queens.

Wachezaji hao ni golikipa, Zubeda Mgunda na beki wa kushoto, Diana Mnally ambao jana walikuwa sehemu ya kikosi ilichofanya mazoezi kwenye Uwanja wa Samora, Iringa kujiandaa na mchezo wao wa Ligi Kuu dhidi ya Ceasiaa Queens.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo imesema imewasajili wachezaji hao ili kukiboresha kikosi hicho, hasa ikizingatiwa wachezaji hao si tu kwamba ni wazoefu kwenye Ligi Kuu, lakini hata kwenye michuano ya kimataifa.

Wachezaji hao wote wawili wamesajiliwa kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili kutoka kwenye timu ya Get Program yenye maskani yake jijini Dodoma inayocheza Ligi Kuu.

Wachezaji hao waliichezea Simba Queens msimu uliopita, lakini waliachwa mwishoni mwa msimu, kabla ya kujiunga na timu hiyo ya Dodoma na sasa wametua Yanga Princess.

**Wakati Zubeda akiitumia Simba Queens kwa muda mrefu, Mnally, aliichezea kwa misimu miwili, am bapo kabla ya hapo ali wahi kuzichezea klabu ya JKT Queens na Fountain Get Princess.**

Shirikisho la Mpira wa Miguu (TFF), limefungua dirisha la usajili kuanzia Desemba 15, mwaka jana hadi Januari 15 mwaka huu ambapo klabu mbalimbali za Ligi Kuu, Ligi ya Championship na Ligi ya Wanawake na timu za Ligi za Mikoa.

Tayari timu mbalimbali zikiwamo za wanawake zimeanza kusaka wachezaji ambao wanaona watawafaa kwa ajili ya kuboresha vikosi vyao kuelekea kwenye mzunguko wa pili wa ligi hizo.

# SINGIDA YAMPATA KOCHA WA ROBO FAINALI TATU CAF

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Singida Black Stars, imemtangaza rasmi, Hamdi Miloud, kuwa Kocha Mkuu, atakayekinoa kikosi hicho akichukua nafasi ya Patrick Aussems iliyomtimua mwishoni mwa mwezi Novemba na msaidizi wake, Denis Kitambi.

Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Hussein Masanza, amesema jana kuwa kocha huyo atachukua nafasi ya Aussems, akiwa na wasaidizi wake wawili, mmoja akija naye mwenyewe, Nassim Anisse, mwingine ni David Ouma ambaye aliteuliwa kushika nafasi hiyo baada ya benchi la mwanzo kuvunjwa.

Taarifa ya Klabu hiyo imeeleza kuwa aliyekuwa anakaimu nafasi hiyo, Ramadhani Nsanzurwimo amerejea kwenye majukumu yake ya awali kama Mkurugenzi wa Ufundi.

Masanza amesema kocha huyo ana uzoefu mkubwa katika soka la Afrika kwa kuzinoa klabu mbalimbali kwa mfanikio makubwa.

Timu alizozinoa kocha huyo mwenye uraia wa nchi mbili za Ufaransa na Algeria, ni USM Alger na JS Kabylie za Algeria, Al-Salmiya ya Kuwait, TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Athletico Marseille na ES Vitrolles za Ufaransa na Al- Ettifaq FC ya Saudia Arabia.

Rekodi zinaonyesha kuwa katika kazi yake ya soka, amefanikiwa kufika robo fainali tatu za michuano ya kimataifa Afrika, akifanya hivyo akiwa na JS Kablie mara mbili kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika na USM Alger katika Kombe la Shirikisho la Soka Afrika.

Wakati timu hiyo ikichukuliwa kutoka Mbarali Mbeya, ikiitwa Ihefu FC katikati ya msimu uliopita, ilikuwa inanolewa na Mecky Maxime, lakini baadaye ilimchukua kocha wa zamani wa Simba, Aussems, huku Maxime akitimkia Dodoma Jiji.

Baada ya kuondoka kwa kocha huyo ambaye aliondolewa baada ya kutofanya vyema kwa baadhi ya michezo mfululizo, ilipofungwa bao 1-0 dhidi ya Yanga, suluhu dhidi ya Coastal Union, sare ya mabao 2-2 dhidi ya Tabora United na kipigo cha mabao 2-1 dhidi ya Azam FC, Nsanzurwimo alipewa jukumu la kukinoa kikosi hicho kwa muda.

Singida Black Stars inashika nafasi nne katika msimamo wa Ligi Kuu ikiwa imeshacheza michezo 16, ikishinda 10, sare tatu na kupoteza michezo mitatu, ikifikisha pointi 33.

Wakati huo huo, Masanza amesema imewarejesha kundini wachezaji, Mourice Chukwu aliyekuwa kwa mkopo Tabora United, Fikirini Bakari kutoka Fountain Gate na Ernest Malonga aliyekuwa kwa mkopo Coastal Union.

"Hawa ndiyo tumewarudisha na wameanza mazoezi, kama kuna wengine watakuwapo basi tutawaambia," alisema.



Vijana wakishindana jana katika mbio za baiskeli kwenye bonanza la michezo la kufunga mwaka 2024 na kuukaribisha mwaka 2025 lililopewa jina la Dk. Samia/Jumbe Holiday lililofanyika kwenye uwanja wa CCM Kambarage Mjini Shinyanga. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Z'bar Heroes kuelekea Pemba Mapinduzi Cup

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Taifa ya Zanzibar 'Zanzibar Heroes ' inatarajia kuondoka hapa Kisiwani Unguja leo Januari Mosi kuelekea Pemba katika Michuano ya Kombe la Mapinduzi kwa mwaka huu 2025.

Michuano hiyo kwa mwaka huu itaanza Januari 3 na kushirikisha timu za Taifa ambazo ni Mwenyeji Zanzibar, Tanzania Bara, Kenya, Uganda, Burundi na Bukinafaso.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Issa Chiwile, alisema timu hiyo itasafiri na wachezaji 29 huku mchezaji wa 30 Sheikhan Ibrahim hatokuwa sehemu ya kikosi hicho baada ya kutopewa ruhusa na timu yake ya Yanga.

Alisema kwa ujumla timu hiyo inaendelea na programu yake ya mazoezi kama ilivyopangwa na benchi la ufundi chini ya Kocha Mkuu Hemed Morocco.

Alisema wachezaji wana ari na hamasa kubwa kama ilivyo kwa wadau wa soka hapa Zanzibar ambao wangi wao wamejitolea kununua jezi za Zanzibar Heroes tayari kuishangilia timu hiyo.

"Benchi la ufundi linaendelea na maandalizi ya mwisho ambayo yatafanyika huko Kisiwani Pemba ili kujiandaa na michuano hiyo ya Kombe la Mapinduzi, kikubwa wachezaji wapo na morali na hamasa kubwa, tunaamini tutafanya vizuri," alisema Chiwile.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa na Kamati ya Kombe la Mapinduzi, wenyeji Zanzibar watafungua mashindano hayo dhidi ya Burundi mchezo utakaochezwa saa mbili na robo usiku katika Uwanja wa Gombani, Pemba.

HABARIMICHEZO

## ZISIKUPITE

### OLMO AGEUKA LULU EPL

JARIBIO la Barcelona lililoshindwa la kumsajili mshambuliaji wa Hispania, Dani Olmo kwa kipindi cha pili cha msimu limefungua milango kwa Manchester United na Manchester City kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 bila malipo.***(Mundo Deportivo)***

### ARNOLD KUSAJILIWA JANUARI

REAL Madrid ingependelea kumsajili beki wa kulia wa England, Trent Alexander-Arnold Januari, lakini wako tayari kusubiri hadi msimu wa majira ya joto wakati mkataba wake utakapomalizika ikiwa Liverpool hawataki kumuuza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 mwezi ujao.***(Marca)***

### ISAKA KUBAKI NEWCASTLE

MSHAMBULIAJI wa Newcastle United raia wa Sweden, Alexander Isak yuko tayari kubakia katika klabu hiyo iwapo watamaliza katika nafasi nne za juu kweye Ligi Kuu msimu huu, na kutoa pigo kwa Arsenal ambao wana nia ya kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25. ***(Sun)***

### CHELSEA YAMTAKA LIAM DELAP

CHELSEA inamfuatilia mshambuliaji wa Ipswich, Liam Delap mwenye umri wa miaka 21, na mshambuliaji wa Brighton wa Jamhuri ya Ireland, Evan Ferguson mwenye miaka 20 wakati wanatazamia kutoa ushindani kwa mshambuliaji ambaye ni chaguo la kwanza, Nicolas Jackson. ***(Talksport)***

### LOPETEGUI KUPEWA MUDA ZAIDI

KOCHA wa West Ham, Julen Lopetegui atapewa muda zaidi licha ya kiwango kibovu cha wagonga nyundo hao msimu huu. (Telegraph)

### RONALDO UWENDA AKAONDOKA

CRISTIANO Ronaldo amekataa kuthibitisha kama hataondoka Al-Nassr msimu wa kiangazi huku mshambuliaji huyo wa Ureno mwenye umri wa miaka 39 akiwa huru kufanya mazungumzo na klabu nyingine kuanzia Januari 1. ***(Marca)***

### TRAFFORD ATAKIWA NEWCASTLE

NEWCASTLE United inapanga kumnunua kipa wa Burnley mwenye umri wa miaka 22, James Trafford kwa kitita cha pauni milioni 20. ***(Sun)***

### DONSO AWANIWA WOLVES

KLABU ya Wolves inataka kumsajili mlinzi wa Lens na Austria, Kevin Danso mwenye umri wa miaka 26 Januari. ***(Sky Sports)***

### MCATEE ATAKIWA UJERUMANI

BAYERN Leverkusen ni miongoni mwa klabu kadhaa zinazomtazama kwa karibu kiungo wa kati wa Manchester City, mwenye umri wa miaka 22, James McAtee. ***(Mail)***


### WERNER KUREJEA RB LEIPZIG

KLABU ya Tottenham Hotspur haina uwezekano wa kubadilisha mkataba wa mkopo wa mshambuliaji wa Ujerumani, Timo Werner mwenye umri wa miaka 28 kwa mkataba wa kudumu, na hiyo inamaana kwamba atarejea RB Leipzig msimu wa kiangazi ***(Bild)***

### SAINZ ATAKIWA ATHLETIC

KLABU ya Athletic Bilbao imemtambua kiungo wa kati wa Norwich, Borja Sainz mwenye umri wa miaka 23, kama kiungo mbadala bora wa Nico Williams iwapo winga huyo wa Hispania mwenye umri wa miaka 22 ataondoka katika klabu hiyo msimu wa kiangazi. ***(Sport)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# BARCELONA YAGONGA MWAMBA KWA OLMO

Mahakama yakataa maombi ya klabu hiyo na sasa Olmo anaweza ku...

**BARCELONA, Hispania**

RUFANI ya Barcelona ya kukataliwa kwa awali ombi lao la kuongezewa muda wa usajili wa Dani Olmo imekataliwa.

Alisajiliwa awali kupitia mwanya wa kukosekana kwa Andreas Christensen ambaye ni majeruhi na usajili wa sasa wa Olmo ulimalizika jana Desemba 31.

Pia ule wa fowadi chipukizi Pau Victor, na kwa hali ilivyo, klabu hiyo haina fedha za kutosha kuongeza usajili wa Olmo. Wiki iliyopita mahakama ilikataa jaribio lao la kufanyia kazi sheria za kifedha za LaLiga.

Mkataba wa Olmo unajumuisha kipengele kinachomruhusu kuondoka kwa uhamisho wa bure ikiwa hawezi kusajiliwa, huku timu kadhaa za Ligi Kuu England zikimuwania.

Sasa, vyombo vingi vimeripoti kushindwa kwa rufaa ya Barcelona, huku mahakama ikisisitiza kuwa uamuzi wa kwanza ulikuwa halali na lazima ufuatwe.

Kwa bahati nzuri kwa Barcelona, wana mpango mbadala kwani uuzaji wa sehemu ya viti vya VIP wa euro milioni 120 pale Camp Nou katika miaka 20 ijayo tayari umekubaliwa na sasa unahitaji idhini ya mwisho.

Mkataba kama huo unatarajiwa kuwapa Barcelona fedha zinazohitajika kuwasajili Olmo na Victor katika kikosi cha kocha Hansi Flick kwa kipindi cha pili cha msimu, na kuwarudisha kwenye sheria ya matumizi ya LaLiga.

# HABARI MICHEZO

## AC Milan wamtimua kocha, wamchukua wa Porto

**MILNA, Italia**



AC Milan imethibitisha kumfuta kazi Paulo Fonseca na wamemteua kocha wa zamani wa Porto, Sérgio Conceição kama kocha wao mkuu wa klabu hiyo kwa mkataba wa miaka miwili na nusu.

Fonseca alikuwa ametangaza kuondoka katika klabu hiyo mapema Jumatatu asubuhi alipokuwa akiondoka kwenye uwanja wa San Siro baada ya sare ya 1-1 ya Milan na AS Roma.

"Ndiyo, ni kweli. Nimetoka," alisema Fonseca akiwaambia waandishi wa habari aliposhusha kioo cha gari lake kuongea nao.

"Hayo ndiyo maisha.., nilifanya kila nililoweza."

"AC Milan inatangaza kwamba Sérgio Paulo Marceneiro da Conceição ameteuliwa kuwa Kocha Mkuu wa kikosi cha kwanza hadi Juni 30 mwaka 2026," ilisema taarifa ya Milan.

Milan itacheza na Juventus katika nusu fainali ya Super Cup ya Italia huko Saudi Arabia Ijumaa hii.

Fonseca aliajiriwa Juni mwaka huu na alisimamia ushindi mara 12 katika mechi 24 katika mashindano yote.

Milan wako katika nafasi ya nane kwenye msimamo wa Serie A, wakipitwa na viongozi Atalanta na Napoli kwa pointi 14.

Wamefanya vyema katika Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya ushindi mara nne mfululizo, ukiwamo ushindi wa 3-1 dhidi ya Real Madrid.

Wako katika nafasi ya 12 na wako mbioni kufuzu kwa raundi ya mtoano.

Conceição, ambaye alicheza Serie A katika klabu za Lazio, Parma na Inter Milan, aliifundisha Porto kwa misimu sita kabla ya kuachia ngazi Juni.

## Ancelotti hana mpango na AS Roma

**ROME, Italia**

CARLO Ancelotti amethibitisha kuwa anataka kubaki kuwa kocha wa Real Madrid kwa "muda mrefu iwezekanavyo".

Kwa muda mrefu Madrid wamekuwa wakitajwa huwenda wakaachana na Ancelotti mwishoni mwa msimu huu, huku bosi wa Bayer Leverkusen, Xabi Alonso akidaiwa kutaka kupewa nafasi hiyo.

Ripoti hizo zikimtaja Ancelotti kuwa anaweza kuchukua mikoba ya kuinoa AS Roma.

"Kuna mazungumzo mengi kuhusu Roma, lakini niko sawa hapa na nitajitahidi kukaa muda mrefu iwezekanavyo," alisema.

"Kocha wa Roma (Claudio Ranieri) ni rafiki yangu na anaendelea vizuri sana, nina furaha naye.

"Nina uhusiano mzuri na Roma, kumbukumbu nzuri sana, lakini kuna safari ndefu ya kusema nakwenda pale.

"Kwa sasa niko vizuri hapa na sifikirii kuhusu maisha yangu ya baadaye, bado nina miaka miwili kwenye mkataba wangu, lakini mikataba inaweza kuvunjwa au kuongezwa."

Hapo awali Ancelotti aliapa kutoongoza klabu nyingine wakati kibarua chake na Madrid kitakapofikia kikomo, ingawa kwa muda mrefu amekuwa akihusishwa na mpango wa kuhamia timu ya taifa, huku Brazil ikijulikana kwa mshabiki wake.



# MAN UNITED SASA YAPAMBANIA KUTOSHUKA DARAJA

**MANCHESTER, England**

RUBEN Amorim amekubali Manchester United iko kwenye vita ya kutoshuka daraja baada ya kichapo cha mabao 2-0 kutoka kwa Newcastle United na amekiri kwa kusema "nia yangu ni ni kuinusuru."

United ilipata kipigo cha nne mfululizo katika michuano yote na kupoteza mechi tatu mfululizo kwenye Ligi Kuu England uwanja wa Old Trafford Jumatatu usiku.

Kichapo hicho kimekiacha kikosi cha Amorim katika nafasi ya 14 kwenye msimamo, pointi saba pekee juu ya nafasi za kushuka daraja.

"Nadhani timu imepotea kidogo kwa wakati huu, kwa hiyo ni aibu kidogo kuwa kocha wa Manchester United na kupoteza michezo mingi," alisema Amorim.

"Lakini lazima tukabiliane na nyakati ngumu katika maisha ya kila mtu, kwa hiyo ni wakati mgumu.

"Nadhani watu wamechoshwa na visingizio katika klabu hii na nadhani wakati mwingine nazungumzia kushuka daraja kwa sababu hiyo.

"Lazima tutambue msimamo wetu kama unavyoona ligi, kwamba kila mtu anaweza kumshinda kila mtu, kwa hiyo lazima tushinde michezo na kuzingatia kunusurika."

United walikuwa nyuma kwa 2-0 ndani ya dakika 20 za kwanza dhidi ya Newcastle kwa mabao ya Alexander Isak na Joelinton.

Amorim alijibu kwa kumtoa Joshua Zirkzee baada ya dakika 33 pekee huku Mholanzi huyo akizomewa vikali na mashabiki wa nyumbani alipokuwa akitoka nje.

"Ulikuwa wakati mgumu sana kwa Zirkzee na yeye ni binadamu," alisema Amorim.

"Mimi ninawajibika, unapokuwa na nyakati za aina hii, haswa katika klabu kubwa, unafanya bidii sana kubadilisha mambo, haswa wakati huna muda mwingi wa kufanya mazoezi ya msingi ili kukabiliana na nyakati ngumu.

"Ni wakati mgumu sana na lazima tupigane kwa ajili ya mchezo unaofuata na kutekeleza wazo la kushinda michezo. Nadhani ni ngumu sana kwa kila mtu na unaweza kuhisi ukiwa uwanjani.

# AZAM KUCHEZA MECHI ZA KIRAFIKI

**Na Faustine Feliciane**

UONGOZI wa klabu ya Azam FC umewapa mapumziko mafupi wachezaji na benchi la ufundi la timu hiyo huku wakipanga kucheza michezo kadhaa ya kirafiki pindi watakaporejea kwenye majukumu yao.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hasheem Ibwe, amesema mapumziko waliyopewa wachezaji ni mafupi na wanatarajia kurejea kwenye majukumu yao wiki ijayo.

Alisema mara watakaporudi pamoja na programu za mazoezi pia wanatarajia kucheza michezo miwili mpaka minne ya kirafiki kujiweka sawa kuelekea kwenye michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Kwa upande wetu kila kitu kinaenda sawa, wachezaji na benchi la ufundi wapo kwenye mapumziko mafupi, lakini mambo mengine yanaendelea, kocha wetu ametoa programu yake ya mazoezi pindi wachezaji watakaporejea, la zaidi pia kuna michezo ya kirafiki tutacheza kabla ya kurejea kwenye Ligi Kuu," alisema Ibwe.

Aidha, alisema pia wamepokea mialiko kutoka baaadhi ya nchi kwa ajili ya kwenda kucheza michezo ya kimataifa ya kirafiki.

Bila kutaja majina ya klabu, ametaja mialiko hiyo inatoka kwenye nchi za Afrika Kusini, Qatar, zambia na Dubai.

"Uongozi na benchi la ufundi utaangalia kama kuna ulazima wa sisi kwenda huko, kama hawataona ulazima basi tutaendelea na programu ya mwalimu wetu," alisema Ibwe.

Kuhusu dirisha dogo la usajili, Ibwe amesema uongozi umepokea mapendekezo ya mwalimu juu ya wachezaji na kuwaacha na wale wa kuchukuliwa kuongoza nguvu kwenye timu hiyo.

"Taratibu zikishakamilika tutatangaza nani na nani tunaagana nao na nani tutawaongeza, kwa sasa kila kitu kinafanyiwa kazi," alisema Ibwe.

Azam FC inashika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi ikiwa na pointi 36 baada ya kucheza michezo 16 ikizidiwa pointi nne na vinara Simba ambao wamecheza michezo 15.




Mshambuliaji wa Simba Queens, Elizabeth Wambui (katikati), akipongezwa na nyota wenzake, Vivian Corazone (kushoto) na Jentrix Shikangwa baada ya kuifungia timu yao bao kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya Wanawake dhidi ya Alliance Girls kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jana. **PICHA: SIMBA**

# Bodi ya Ligi yaridhishwa mzunguko wa kwanza

**Na Faustine Feliciane**

BODI ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB) imesema imeridhishwa na mwenendo wa ligi hiyo kwenye mzunguko wa kwanza uliokamilika hivi karibuni.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Ofisa Mtendaji Mkuu wa bodi hiyo, Almas Kasongo, alisema licha ya mapungufu madogo yaliyoonekana lakini kwa ujumla ligi hiyo imeenda vizuri.

Kasongo, alisema mabadiliko ya ratiba ndio kitu pekee ambacho kimeenda tofauti na mipango yao msimu huu.

"Yale ambayo tulikuwa tumeyapanga kabla ya kuanza kwa Ligi Msimu huu wa 2024/2025 kwa kiasi kikubwa yameenda sawa kama tulivyotaka, utofauti kidogo ni kwenye ratiba kutokana na uwepo wa mashindano ya Mapinduzi na CHAN," alisema Kasongo.

Aidha, alisema TPLB pia inaridhishwa na ushindani uliopo kwenye ligi baina ya klabu kwa klabu.

"Tunaona ushindani uliopo, kila timu inapambana kuhakikisha inapata alama tatu, na sisi ndicho ambacho tunakitaka, hii inafanya ligi kuwa yenye ushindani sana," alisema Kasongo.

Wakati huo huo, baada ya kusambaa taarifa kuwa klabu yaSimba imeandika barua kwa TPLB kuomba kuhama uwanja kutoka KMC na kurejea Azam Complex, ofisa habari wa bodi hiyo, Karim Boimanda, amesema hakuna barua iliyoandikwa na Simba juu ya taarifa hiyo.

"Hatuna taarifa hizo rasmi, tunasikia tu kwenye mitandao, na inawezekana mtu tu kaamua kuanzisha hiyo ajenda, lakini hatuna barua rasmi kutoka Simba wakiomba kuhama uwanja," alisema.

Aidha, alisema mpaka sasa bodi hiyo inatambua uwanja wa nyumbani wa Simba ni KMC Complex.

## Ramovic: Mchezo na TP Mazembe

INATOKA UK. 24

watakuwa wamejiweka katika mazingira magumu kutinga robo fainali ya michuano hiyo kwa mara ya pili kwani watabakiwa na pointi moja huku Mazembe wakiwa na pointi sita.

Yanga wakishinda watakuwa wameamsha matumaini ya kusonga mbele kwa kuwa watakuwa wamefikisha alama nne na kutakiwa kushinda mechi mbili zitakazokuwa zimebaki dhidi ya Mc Alger na Al Hilal.

## Simba yapaa kufuata pointi tatu Tunisia

INATOKA UK. 24

nne zina uhakika wa kwenda robo fainali, timu tatu zinafanana kwa pointi, mechi yetu dhidi ya CS Sfaxien ndiyo itaanza kuonyesha utofauti nani awe kwa kwanza na nani wa pili kwenye kundi yupi wa tatu na yupi abaki mkiani.

Kwetu Simba huu mchezo ndiyo unakwenda kutengeneza dira au taswira ya kuelekea hatua ya robo fainali, ni mechi ngumu kwa sababu mpinzani wetu anataka kuifanya mechi hii kwake iwe na kuamkia. Ni muhimu kwetu kwenda na nguvu zote kuhakikisha tunapata ushindi katika mchezo huu, tukishinda tutakuwa tumemwondoa kabisa CS Sfaxien katika mbio za kuwania robo fainali na kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kufuzu kutoka kwenye Kundi A," alisema Ahmed.

Alisema kuwa, si kwa Sfaxien tu, pia wamejizatiti kutopoteza mechi nyingine dhidi ya Bravo do Maquis ya Angola na CS Constantine ya Algeria.

Simba iko Kundi A, ikiwa nafasi ya tatu katika msimamo, ikikusanya pointi sita sawa na kinara wa kundi, Bravo do Maquis na CS Constantine ambayo ipo nafasi ya pili lakini zikitofautiana mabao ya kufunga.

Bravo do Maquis ina mabao sita, CS Constantine ikifunga matano, huku Simba ikifunga manne, CS Sfaxien ikiwa haina pointi.

Wakati huo huo, Ahmed, alisema tayari winga, Elie Mpanzu amekamilisha usajili kwenye michuano ya kimataifa, hivyo atakuwapo kwenye mchezo huo.

Mpanzu ambaye tayari ameshaanza kukipiga kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya taratibu zake kukamilika, amekamilisha pia usajili kwa ajili ya Kombe la Shirikisho.

"Nawatoa wasiwasi wanachama na mashabiki wa Simba kuhusu Mpanzu, taratibu zote za kucheza michuano ya kimataifa nayo pia imekamilika kwa hiyo atakuwa mmoja wa wachezaji watakaoenda kutuwakilisha nchini Tunisia," alisema.

# Michezo

Jumatano Januari 1, 2025

Nipashe


**Barca yagonga mwamba kwa Olmo**

UKURASA 21





Golikipa wa Manchester United, Andre Onana, akiruka juu kuzuia mpira kwenye msitu wa watu wakati wa mchezo wa Ligi Kuu ya England dhidi ya Newcastle juzi kwenye Uwanja wa Old Trafford, United ilifungwa mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA YAPAA KUFUATA POINTI TATU TUNISIA

Yaondoka na msafara wa watu 50, yajipanga kuhakikisha wana...

**Na Adam Fungamwango**

MSAFARA wa watu 50 wakiwamo wachezaji 22 wa timu ya Simba, ulitarajiwa kupaa saa 10:00 alfajiri ya leo kuelekea nchini Tunisia kwa ajili ya mchezo wao wa raundi ya nne, Kombe la Shirikisho Afrika hatua ya makundi dhidi ya CS Sfaxien, huku Meneja Habari wa Klabu hiyo, Ahmed Ally, akisema hawahitaji matokeo mengine zaidi ya ushindi kwenye mchezo huo.

Simba ambayo itapitia nchini Uturuki kabla ya kwenda Tunisia, inatarajiwa kucheza mechi hiyo Jumapili ijayo Januari 5 kwenye Uwanja wa Olympique Hammadi Agrebi kwenye mji wa Rades saa 1:00 usiku kwa saa za Tanzania.

Ahmed, alisema matokeo ya mchezo huo ndiyo yatatoa dira na taswira ya kuelekea kwenye hatua ya robo fainali au la.

Alisema ugumu wa mchezo huo utatokana na kwamba CS Sfaxien wanataka kuutumia mchezo huo ili kurudi kwenye njia baada ya kupoteza michezo yake yote mitatu iliyopita.

"Kundi ni gumu kwa sababu timu zote

INAENDELEA UK. 23

## Ramovic: Mchezo na TP Mazembe ni hatima yetu Ligi ya Mabingwa

**Na Faustine Feliciane**

KOCHA wa Yanga, Sead Ramovic, amesema mchezo wao wa Jumamosi ijayo dhidi ya TP Mazembe utaamua hatima yao kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika huku akiwaomba mashabiki kuujaza uwanja.

Jumamosi, Januari 4, Yanga itaumana na Wakongo hao kwenye mchezo wa marudiano hatua ya makundi huku wawakilishi hao wa Tanzania wakihitaji ushindi kuweka hai matumaini ya kutinga hatua ya robo fainali.

Akizungumza juzi jijini Dar es Salaam, Ramovic, amesema kutokana na umuhimu wa mchezo huo angependa kuona mashabiki wanajitokeza kwa wingi kuwaongezea hamasa wachezaji wake ili kupata kile wanachokihitaji.

"Ni mchezo ambao tunahitaji ushindi sana, hatima ya sisi kuendelea kupambania kuchezea robo fainali ni kwenye mchezo huu na TP Mazembe, tutaendelea na maandalizi yetu mpaka siku ya mchezo," alisema Ramovic.

Aidha, alisema mchezo huo hautakuwa mwepesi kutokana na wapinzani wao nao kuhitaji ushindi.

„Tulifanikiwa kupata alama moja ugenini, TP Mazembe watakuja kwa lengo la kupata ushindi na wao, lakini sisi kuwa kwenye uwanja wa nyumbani utachangia sana kupambana kupata ushindi," alisema Ramovic.

Aidha, kuhusu maandalizi yao, Ramovic, amesema baada ya kuwaona wapinzani wao kwenye mchezo wa kwanza Lubumbashi ambao ulimalizika kwa kufungana bao 1-1, vipo vitu anavyoviongeza kwa wachezaji wake mazoezini.

"Utakuwa mchezo wa mbinu zaidi, yapo mambo ambayo nayafanyia kazi ili kuhakikisha tunapata ushindi, nimewaona wapinzani wetu ni timu nzuri na yenye uzoefu sasa lazima tujipange vizuri," alisema.

Kwenye kundi lao la A la michuano hiyo, Yanga wanaburuza mkia kwa kuwa na pointi moja pekee katika michezo mitatu waliyocheza, Al Hilal wanaongoza wakiwa na pointi tisa wakifuatiwa na Mc Alger wenye pointi nne huku TP Mazembe wakiwa nafasi ya nne na pointi mbili. Kama Yanga watapoteza mchezo huo

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >